

MUNGU AKIJIFICHA

KATIKA URAHISI



Asante, ndugu. Habari za jioni. Ni majaliwa kuwa hapa, usiku huu, katika wakati huu mzuri wa ushirika. Linaonekana ni jambo halisi sana, kupata kusikia shuhuda za watu wengine ambao wanafurahia baraka hizi nzuri sana, ambazo tunashirikiana pamoja matukio yetu juu yake, usiku wa leo. Na sasa mimi, pia, ninataka kumshukuru Ndugu Shakarian, na wengi wa nanii... huyu Ndugu Danny, na wengine wengi sana ambao wapo hapa, ambao siwezi kukumbuka majina yao, kwa kunialika hapa kwenye tawi hili zuri ha—hapa Alburqueque.

² Ninafikiri ya kwamba kama tungeninii, wakati mwingine, katika kuanzisha tawi lenu lingene, kama mngemtuma mtu huko, na kwa namna fulani ayazungukie makanisa, ufufuo mdogo, awahimize waombe, na kukesha, na wawe katika matarajio makanisani, na Roho wa Mungu akitenda kabisa, na kisha aingie katika mojawapo ya ninii hizi, ndipo kwa kweli tu unakua na kitu fulani. Sisi...

Mna matumaini ya kufanikiwa hapa. Mna—mna watu walio madhubuti.

³ Ninakuta, kokote niendako, nimezuru huku, kwa kiasi fulani sasa, kwa miaka michache iliyopita, pande zote, pande zote ulimwenguni, nikihubiri. Na ninaona ya kwamba, kila mahali, Mungu ana watu madhubuti katika ujuzi huu wa ajabu. Ninaenda huko ndani katika misitu ya Afrika, na India, huko visiwani, ninakuta watu ambao hata hawajui mkono wa kulia na wa kushoto ni upi; hawajawahi kusikia Jina la Bwana Yesu; hawajui chochote kuhusu Hilo, hata kidogo. Na jambo la kushangaza, wanapompokea Roho Mtakatifu, wanafanya vile vile kabisa kama mnavyofanya sasa. Unaona? Wao... Mnaweza kuona kwa—kwa kweli ni kitu halisi. Na Mungu anawapenda, anawaponya.

⁴ Sasa, tawi hili la wafanyabiashara, ndicho kitu pekee ninachoshirikiana nacho, kadiri mashirika ya ulimwengu huu yanavyohusika. Ni kwa sababu ya jambo hilo, wakati mmoja nilikuwa ninii...

⁵ Tulikuwa tumeketi pale, mimi na Ndugu Crow, tukizungumza juu ya msingi wetu wa Kibaptisti. Mimi niliwekwa kuwa mhudumu, kwenye kanisa la Kimishenari la Kibaptisti. Lakini basi, bila shaka, wakati hilo tukio lilipokuja, la Roho Mtakatifu, vema, hilo lilimaliza jambo hilo papo hapo.

Na kwa hiyo sisi...Sina kitu dhidi ya hao ndugu walioko kule. Kuna watu wazuri kwenye kundi lile, na miongoni mwa makanisa yote, madhehebu yote. Lakini tunawathamini sana.

⁶ Huu umekuwa ni wakati mzuri sana kwangu. Hili la Wafanyabiashara limekuwa ndicho kitu ambacho mimi... kimenipa mahali pa kuhubiria.

⁷ Sasa, niliposikia jina, 'pentekoste,' mbona, nililisikia jina hilo, nao wakaniambia, 'Lilikuwa ni kundi la watakatifu wanaojifingirisha wanaojifingirisha huku na huko sakafuni, wakitokwa na mate tele—na kila kitu.' Lakini ni—niliona ya kwamba si kweli.

⁸ Na basi, lakini wakati nilipofika, nilipokuja miongoni mwao, wao walikuwa—walikuwa wamegawanyika madhehebu mengi mbalimbali kama sisi Wabaptisti tulivyokuwa nayo. Ninii tu, walikuwa tu...Nilifikiri walikuwa kundi moja tu. Lakini nikaja kuona, kuna makundi ya kila aina, wakizozana moja kwa lingine vibaya tu karibu kama sisi Wabaptisti na wengine wetu. Na tuko karibu sawa nao.

⁹ Halafu basi—basi, badala ya kuingia na kujiunga na aidha Assemblies, au na Waunited, ama na wa kanisa la Mungu, na watu wote hao ni wazuri sana, makundi hayo yote, nilisimama tu kati yao, na kusema, "Sisi ni ndugu. Msibishane, mmoja kwa mwingine." Sasa, kama Shetani anaweza kutufanya tuendelee kupigana sisi kwa sisi, haitambidi kupigana. Unaona? Lakini wakati tunapolenga bunduki zetu kwake, na kuacha kulengana mmoja kwa mwingine, tukapendana sisi kwa sisi, tukifanya ushirika sisi kwa sisi, basi ule Utawala wa Miaka Elfu utanza.

¹⁰ Lakini hilo limekuwa ndilo kusudi langu. Na kundi hili la Wafanyabiashara wa Full Gospel hapa limekuwa ndio mahali pangu pa mapumziko, pa kukusanyika pamoja. Kwa sababu, nao wanadhamini mikutano yangu mingi. Na kwa njia hiyo ni—ninii...Watu wao. Ili kulinda heshima zao, inawalazimu kuingia, unaona, kwa hiyo li—limenifanyia jambo kubwa hapa katika taifa hili, katika Marekani hii.

¹¹ Sasa, ya 5, ya 6, ninajua ya kwamba mimi...je! ni sawa kusema jambo fulani kuhusu mkutano? [Ndugu fulani anasema, "Hakika."—Mh.] Naam. Kulikuwa na Juni 5, 6, na 7; 5, 6, 7 na 8, tuna uamsho huko Tucson, mahali pale ambapo wanafanyia dhi-...Dhifa ya Wafanyabiashara. ["Hoteli ya Ramada."] Hoteli ya Ramada. Inakaa yapata watu elfu mbili mia tana, elfu tatu mia tano, yote imeyoyozwa.

¹² Na sasa, mimi kama msemaji, mtu yeyote anayenijua, anajua ya kwamba mimi si msemaji. Nina elimu ya—ya shule ya msingi tu, na hiyo ni elimu ndogo. Nilifikia tu darasa la saba. Na kwa hiyo mimi, kuhusu kusema, 'mhubiri,' mnajua mimi si mhubiri. Bali ninamfanyia Bwana kelele za furaha, na kisha ninajaribu kushiriki yale niliyojifunza juu Yake, pamoja na wengine.

¹³ Wito wangu maishani ni maombi kwa wagonjwa, kuwaombea wagonjwa. Hicho ndicho Bwana amenibariki nacho, mikutano mikubwa, nikiwaongoza watu. Idadi kubwa kabisa niliyowahi kuwa nayo kwa wakati mmoja katika mkutano mmoja, ilikuwa ni kule Bombay, mia tano elfu katika mkutano mmoja.

¹⁴ Na halafu, Afrika, ninaamini, kama tungehesabu waongofu wa wananchi waliovaa mablanketi, makafiri, wasiojua mkono wa kulia ni upi na wa kushoto ni upi, tulikuwa na thelathini elfu kwa wakati mmoja, waliompokea Kristo kama Mwokozi, wakati mmoja. Kuhusu mvulana kiwete na kipofu, asiye hata na akili timamu, mtu wa tano jukwaani. Na wakati Roho Mtakatifu . . .

¹⁵ Nami niliona madaktari wa madawa, kama daktari huyu mzuri wa madawa hapa, muda mfupi uliopita. Kama ningalikuwa katika jiji hili, nikiwa mgonjwa, na ilinipasa kupata matibabu ya mwili, ningetaka mtu kama huyo kunitibu, mtu anayemwamini Mungu. Kama ingenibidi kupata msaada wake wa madawa, hakika ningetaka mtu ambaye anamwamini Mungu namna hiyo. Ninii halisi . . . Ninyi mna bahati hapa, katika jiji hili, kuwa na daktari kama huyo, mtu mcha Mungu halisi, ambaye anamtumaini Mungu kwa kazi yake ya upasuaji, ama chochote anachofanya. Ni—nina imani katika mtu kama huyo. Nimewaona madaktari wa madawa wakija na—na kuitoa mioyo yao kwa Kristo, kisha wakawa wamishenari huko kwenye misitu. Nami ha—hakika nathamini jambo hilo.

¹⁶ Sasa hapa, na huko nyumbani Marekani, ninasafiri kila mahali, ninafanya ibada ndogo ya uponyaji, nawaombea watoto wa Mungu walio wagonjwa. Nami ninathamini nafasi hiyo, sana.

¹⁷ Kwa hiyo kama uko, kule, karibu na Tucson, tarehe 5, 6, 7, na 8 Juni, tawi la huko litaudhamini, kwa sasa, kadiri tujuavyo sisi. Na makusanyiko yote ya Assemblies of God, nafikiri kuna Assemblies of God tano, sita, ama saba. Na mengi ya hayo mengine, kanisa la Mungu, na kadhalika, yote yanakuja kwa ushirika wa pamoja kwa ajili ya mkutano huu. Sasa, kama wewe . . . kama . . . nafikiri umetangazwa. [Ndugu fulani anasema, “Uko huko katika Hoteli ya Ramada tena.”—Mh.] Utakuwa kwenye Hoteli ya Ramada. Ndugu Stromei, si—sijui jinsi ya kuliendeleza, bali yeye ni ninii . . . Mnaliona kwenye gazeti la *Sauti ya Wanaume* pale. Angeweza kuwaelezea vizuri zaidi juu yake, wakati unapoendela.

¹⁸ Ninaondoka sasa, mara moja, kwenda Alaska, kuandaa mkutano huko Anchorage.

¹⁹ Na kwa hiyo basi ninaenda huko Yukon, kama juma lingine ama siku kumi, na huko mahali padogo pa ndani ndani. Ambako, wahudumu, kama vile watu mashuhuri, kama Ndugu Roberts na Tommy Osborn, na baadhi ya watu hao walio na huduma hizo

kuu maarufu, hawawezi kwenda sehemu hizo. Ha—hawawezi kugharimia hilo. Hawawezi kabisa kuchukua wakati kama huo.

20 Vema, nimejaribu kuidumisha, huduma ndogo ambayo Bwana amenipa, ikiwa nyenyekevu. Si—si—sininii... Kamwe sijawahi kuchukua sadaka maishani mwangu. Si—si—sina vipindi vya kudhamini kwenye vyombo vya habari. Si—sina kitu cha kuuza. Ni—ni—ninataka tu kuidumisha hivi kwamba kama—kama Bwana ananitaka niende nikawahubirie watu kumi, ninaweza kwenda. Na kama ananitaka niende katika nchi za ng'ambo, Yeye atadhamini hilo. Kwa hiyo ninaweza kwenda mahali popote anaponiongoza. Kwa namna fulani ni—ninapenda jambo hilo jinsi hiyo. Wala sina haja ya kuwa na pesa nyingi sana, wala chochote kile. Ninataka tu baraka za Bwana. Kwa hiyo ninyi niombeeni tu, mkitaka. Yaani, Nilikuwa nikifikiri wakati Ni... .

21 Si muda mrefu uliopita, nilialikwa na Ndugu yetu Oral Roberts, mtu shujaa na wa thamani. Nilikuwa nimesimama mahali pake kule. Ninaamini alisema iligharimu kama dola milioni tatu, hilo jengo ama kitu kama hicho. Loo, jamani! Mimi nimezuru Hollywood, na nilimwomba Mfalme George katika hiyo ikulu yake, na Gustav huko Sweden, na mahali mbalimbali, na nimezuru sehemu nyingi sana, majaliwa ya kuwa huko, na nimeona mengi, bali sijawahi kuona jengo linalolingana na hilo. Na nilipoingia ndani, kulikuwa na watu wengi sana mlangoni, ilibidi polisi wanitembeze sehemu mbalimbali na kunitoa nje kwa njia ya nyuma, nikingoja, nipate kutoka nje kwa ajili ya kufanya maombi kwa ajili ya wagonjwa. Na wakati nilipotoka kwa upande wa nyuma, Ndugu Fisher ndiye aliyenitoka nje, baada ya kunitembeza nione jengo hilo, wakati nilipokuwa nimesimama huko nje na kuangalia hilo jengo kubwa mno.

22 Nilikuwa tu nimetoka kwa Ndugu Tommy Osborn. Vijana hao wote wawili wanasema walikuja mkutanoni nao wakavuviwa. Ninamshukuru Bwana, basi, kwa kunijalia niwe na sehemu ndogo katika huduma hiyo.

23 Na jinsi ambavyo Ndugu Osborn, jinsi alivyokuja hapo usiku huo, na akamwona huyo mwenda wazimu akikimbia kuja jukwaani, kunia. Naye akatupa mikono yake, na kusema, “Nitavunja kila mfupa mwilini mwako.”

24 Nikasema, “Kwa sababu umemsai Roho wa Mungu, usiku wa leo, utaanguka miguuni pangu.”

25 Akanitemea mate usoni. Kasema, “Nitakuonyesha nitaanguka kwenye miguu ya nani.” Ndipo akainua ngumi yake anipige.

26 Basi nikasema, “Shetani, mwache mtu huyu.” Akazunguka-zunguka kwa kasi, akuzunguka-zunguka, kisha akaanguka miguuni pangu. Na ndipo ikabidi polisi wamfingirishe kumwondoa.

²⁷ Tommy Osborn akasema, “Kama Mungu anaweza kufanya hivyo kwa mtu mmoja, anaweza kufanya hivyo kwa mtu mwingine.” Na kwa hiyo . . .

²⁸ Naye Tommy Osborn, mtu hodari, mwanamume kweli kweli! Nimefika huko kwenye makao yake makuu na kuona jengo lake kubwa.

²⁹ Nikaja huku nikaona Ndugu Oral Roberts. Ndipo wao waka- . . . Nikatoka, kupitia mlango wa nyuma. Walikuwa waje wanichukue. Nilikuwa nikiangalia jengo hilo kubwa, kubwa mno. Nikawazia, “Loo, jamani! Mwangelie Ndugu Tommy, Bwana, jinsi ulivyombariki.” Niliangalia hapa na nikaona la Ndugu Oral. Nikasema, “Hebu wazia yale Mungu anayoweza kumfanya maskini mtu mmoja mnyenyekevu! Oral Roberts, aliyezaliwa katika mtumbwi, nafikiri, huko sehemu fulani. Maskini mvulana mmoja fukara, na angeweza kumpa mamilioni ya dola mikononi mwake, na mambo mengine.”

Sasa, kitu Fulani kikaniambia, “Vema, na wewe je?”

³⁰ Nikawazia, “Vema, hapana.” Nikawazia, “Da! Hakika ningeona aibu mmoja wao akija kwangu. Nina mashine moja ya chapa iliyowekwa kwenye mwisho wa jengo. Sasa, Ndugu Oral alikuwa, ninaamini, na mashine mia tano za IBM kwenye ghorofa moja.” Nikawazia, “Kila kitu hata hakikuguswa na mikono ya binadamu, vimelundikana *hivi*.” Nikawazia, “Loo, Jamani! Kama angekuja kwangu, aseme, ‘Ningependa kuona ofisi yako, Ndugu Branham.’ Salaale!” Nikawazia, “Ningejionea aibu.” Nikawazia, “Vema, Bwana, labda—labda usingeweza kuniamini. Labda nisingejimudu kuwa hivyo.” Nikasema, “La. Bwana, Wewe huna kikomo. Unajua sina akili nyingi kama wao.” Nikawazia, “Angalia yale waliyorithi.” Nikawazia, “Vema, nafikiri sina nyingi.”

³¹ Ndipo kitu fulani kikasema, “Angalia juu.” Basi hapo niliridhika vizuri kabisa. Ninautafuta Mji Ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu.

³² Sasa, sina kitu dhidi ya ndugu hawa ambao Mungu anaweza kuwaamini namna hiyo, bali ni—ninawapenda. Nami ninamshukuru Mungu kwa kufanya jambo hilo kwa watu mashuhuri kama hao.

³³ Lakini, kwangu mimi, jambo hilo lingenikera hata kufa, vema, kama ingalinilazimu kuwa na dola elfu ishirini, thelathini kwa siku, kuendesha shughuli fulani. Kama nikipata za kutosha kwa ajili ya watoto wangu watatu, na mke wangu, na mimi mwenyewe, za kula, na mahali pa kulala, hilo ni sawa kabisa kwangu. Halafu kama Bwana ananitaka niende mahali fulani, sehemu hizi duni za hali ya chini, basi ninaweza kwenda. Labda yeye aliniweka namna hiyo, unaona.

³⁴ Nisingeweza kukutana na watu ambao wao wanakutana nao. Mimi sina akili za jinsi hiyo. Sina elimu hiyo. Kwa

hiyo, ninaenda, ninawaombea watoto Wake walio wagonjwa, na nikitumaini ya kwamba siku moja, katika majumba ya fahari huko Juu, kwamba sisi sote tunaweza kukutana tena, ambako kamwe haitatubidi kuwa wagonjwa, hakuna mikutano mingine ya maombi wala hakuna kuwahubiria wenye dhambi. Mpaka wakati huo, mimi ni ndugu yenu katika Kristo.

³⁵ Sasa, kanda ambazo zinatengenezwa hapa, hizo ni ninii, hizo mnaweza kuzipata kule. Bw. Sothmann, yuko hapa. Tayari zimetengenezwa. Mara tu baada ya ibada, mnaweza kuzichukua. Hamna haja ya kuzingojea. Ziko papo hapo, mnaweza kuzichukua.

Na, sasa, niombeeni.

³⁶ Na sasa, usiku wa leo, Ndugu Shakarian aliniambia alikuwa aniachilie mapema. Nafikiri hilo linamaanisha, “ondoka mapema.” Nami ni—nitajaribu niwezavyo kufanya hivyo. Na kwa kuwa hii ni Ijumaa Kuu, nami nilifikiri, asubuhi ya leo, kuchukua. . .

³⁷ [Ndugu Demos Shakariana anasema, “Ni wangapi wanaotaka Branham achukue tu wakati wake wa maridhawa, haidhuru, asiharakishe?” [Kusanyiko linashangilia na kusema, “Amina.”—Mh.] Loo! Asanteni. Asanteni. Asanteni. Asanteni. Asanteni. [“Vema. Sitaki mnilaumu.”] La, ndugu. Ndugu Shakarian, sikumaanisha jambo hilo jinsi hiyo. Unaona? Mimi. . . [“Tunataka—tunakutaka ujipe muda tu, Ndugu Branham. Tuna usiku mzima hapa.”] Asante. Asante. [“Alipo Bwana, kuna amani, kuna faraja, na kuna raha.”] Asante.

³⁸ Mimi, wakati mwingine, katika kuhubiri, kama nikichanganya maneno yangu, inanikumbusha tu juu ya hadithi moja fupi niliyosikia wakati mmoja, ya mvulana mmoja mdogo. Mhudumu mmoja alikuwa akipanda kuja kwenye—kwenye ujia, naye akamsikia mvulana mdogo pembeni, akikariri alfabeti zake, “A, B, C, D. . .” Naye akamsikiliza. Alikuwa ameinua mikono yake kuelekea Mbinguni. Akasema. . . Baada ya kuzimaliza, akainuka, akavaa kofia yake.

³⁹ Akasema, “Eti Mwanangu?” Akageuka na kuangalia. Akasema, “Mimi ni mhudumu.” Kasema, “Nilikusikia wewe, ukiwa umepiga magoti, umeinua mikono yako, ukikariri alfabeti.”

⁴⁰ Akasema, “Bwana,” akasema, “Nililelewa kwenye nyumba ya Kikristo. Baba na mama waliuawa wote wawili, ghafla. Nikatolewa nje.” Kasema, “Mtu ninayeishi naye ni mkatili sana kwangu!” Kasema, “Nilikuwa tu nikiwombea. Mimi sijui kuomba.” Akasema, “Nilikuwa tu nikikariri alfabeti zote, na nikawazia labda Mungu angefahamu jinsi ya kuziunganisha pamoja.”

⁴¹ Kwa hiyo labda mwazie tu jambo hilo la jinsi hiyo hiyo kwangu, ya kwamba—ya kwamba labda Yeye atafahamu na

kuyaunganisha pamoja kwa njia fulani ambayo mtafahamu kutokana na ku—kusudi na ninii . . . nililo nalo moyoni mwangu kwa yale ninayosema.

⁴² Sijawahi kamwe ku—kujaribu kuwa na wasiwasi miongoni mwa watu, kwa maana nimekuwa miongoni mwa watu. Nina jambo moja tu ambalo ninaona, na hilo ni Kristo. Naye amesulibishwa. Ninaona Kanisa moja ambalo ninapenda, alilolifia. Nami nimekuwa na juhudi sana juu ya kanisa hilo. Nami nina—ninafanya niwezayo kuliweka jinsi ninavyofikiri ni sawa kabisa, kuliambatanisha na Neno la Mungu. Na, sasa, ninatarajia siku moja kuishi Milele isiyo na kikomo pamoja nanyi, huko kwenye Nchi ambayo tutaketi hivi kama tulivyoketi usiku wa leo.

⁴³ Kama vile mara nyingi nikiangalia wakati tunapokuwa na viamshakinywa na vyakula vya jioni, na vitu kama hivyo. Sasa, mimi ni mkazi wa kusini. Na bado ni wakati wa “chakula cha jioni” kwangu mimi. Wanazungumza juu ya kiamshakinywa hiki hapa, chakula cha mchana, na chakula cha kutwa. Si—siwezi kufanya hivyo. Sasa nini kinatokea kwa chakula changu cha jioni? Unaona? Ni—ni—ninaninii tu . . . Sina budi kula chakula changu cha jioni. Hiyo ni kweli. Kula tu chakula cha mchana hakutanifaa kitu. Sina budi kula mara tatu kwa siku.

⁴⁴ Lakini, basi, ninafikiria, nilipoangalia. Nilikuwa nikipeana mikono na baadhi ya watu hawa hapa, wahubiri wazee ambao labda walikuwa kwenye huduma wakati nikiwa bado ni mwenye dhambi. Nami ninawaangalia, kisha ninafikiria kuona hizo mvi kwenye nywele zao. Ninawazia, “Jamani! Hao watu walikuwa huko nje, wakipigana, kabla hata sijaongoka. Sina shughuli ya kusimama hapa jukwaani, nikizungumza na watu wa namna hiyo.” Basi ninaangalia huko nje . . .

⁴⁵ Vema, jambo pekee walilofanya, wa—walitabiri na kusema mambo haya yangekuja. Nami ninataka mjue, enyi ndugu, ninafikiri mlininii tu—mliweka tu mawe ya msingi kwa ajili ya ninii . . . na kuingia hudumani.

⁴⁶ Ninyi ndugu wa kipentekoste mliosimama huku nje mkiwa na tari mkononi mwenu, wakati hamkuwa na kanisa la kuhudhuria, wakati watu walipowacheka na kuwatupia mayai yaliyooza, na mlifungwa gerezeni usiku kucha; mkavunja mahindi kwenye njia ya reli, watoto wenu wakashikwa na njaa. Mungu abariki nafsi zenu shujaa! Mnapaswa kuwa hapa, sio mimi.

⁴⁷ Bali mmesema ya kwamba utakuja wakati ambapo mambo haya yangetukia. Nina furaha kuwaona mkiishi kuyaona yakitukia. Nusu yake haijapata kusimuliwa bado. Nami—nami ninawathamini.

⁴⁸ Ninaangalia huko chini mezani na kuwaona, watu mbalimbali. Ninafikiria, “Inawezekana nisile chakula cha

jioni pamoja nanyi hapa duniani tena. Lakini siku moja, wakati maisha yamekwisha, tutakula chakula cha jioni tena, hiyo ni kweli, huko juu katika Nyumba ya Baba, wakati tutakapoangalia upande wa pili wa meza na kuonana sisi kwa sisi.” Sasa tuko kwenye uwanja wa mapambano sasa. Lazima tuharakishe. Lakini ninawazia tu itakavyokuwa wakati nitakapoangalia upande wa pili wa meza na kuwaona wote waliokombolewa wameketi pale, ninyoshe mkono na kuwapa mkono. Tutaanza kulia. Hatuna budi kulia. Ndipo Mfalme atakuja na kupangusa machozi yote kutoka machoni mwetu, aseme, “Msilie, watoto. Yote yamekwisha. Ingieni katika furaha ya Bwana iliyowekwa tayari kwa ajili yenu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Maskini tofauti zetu zitafifia wakati huo. Na kutakuwako na Milele moja kuu. Ninataka kuiishi pamoja nanyi.

Na tuombe sasa tunapoinamisha vichwa vyetu.

⁴⁹ Baba yetu wa Mbinguni, Yehova mkuu, mwenye nguvu Ambaye alinguruma hapo mwanzo na kusema, “Iwe nuru,” na ikawa nuru. Loo, nguruma tena, Yehova! Angaza Nuru njiani mwetu, usiku wa leo. Liangazie Nuru Neno Lako. Iangazie Nuru siku tunayoishi. Tuma Nuru. Tujalie, Bwana.

⁵⁰ Wabariki watu wako kila mahali kote ulimwenguni, mahali ambako mioto ya uamsho inawaka mbavuni mwa vilima, katika nchi za makafiri kote ulimwenguni. Tunaomba ya kwamba utambariki kila mhudumu aliyetumwa na Mungu. Ee Mungu, yavuvie maisha yao. Wazia tu, katika wakati uu huu, watu wanampokea Roho Mtakatifu kote ulimwenguni. Watu wanaponywa, dakika ii hii, kote ulimwenguni. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya baraka hizi kuu zilizo ulimwenguni kote ambazo zilisababishwa na mauti ya Mwanao, miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, alasiri ya leo, kama tulivyosherehekea, hii Ijumaa kuu.

⁵¹ Tunaomba, Bwana, ya kwamba Roho Wake Mtakatifu atakuja miongoni mwetu sasa, na atatupa ile sehemu ya Mkate wa Uzima tunaohitaji, ambao utatushikilia kwa ajili ya safari nyingine iliyo mbele yetu, tunapokuja kando kutoka kazini, kwa siku hizi chache, kuketi kwenye kivuli cha Mti wa Uzima, kufurahiana sisi kwa sisi na ushirika wetu wa pamoja. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hilo. Limekuwa la kuburudisha. Sasa tujalie, mara nyingine tena, usiku wa leo, Baba, na ujaze nafsi zetu.

⁵² Mponye kila mgonjwa aliyepo hapa. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya uponyaji Wako, leo, wa dada yetu mwenye ule mkono mfupi na mguu mfupi katika hali hiyo. Tunakushukuru, Bwana. Tunakushukuru. Inaonyesha ya kwamba Mungu aliye hai anaishi miongoni mwetu. Tunakushukuru kwa ajili ya yule dada aliyeponywa tezi kooni mwake. Labda hata hatujui bado

yale yote ambayo umefanya. Ni ajabu sana, Bwana kuona jinsi unavyofanya mambo. Tunakushukuru.

⁵³ Sasa tubariki zaidi. Bariki kusomwa kwa Neno Lako. Wafiche watumishi Wako sasa. Tahiri midomo itakayonena, na masikio yatakayosikia, kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁵⁴ Sasa hebu na tufungue kwenye somo letu tusome, ama kwa ajili ya kusoma Maandiko, hasa. Ninataka kusoma katika mahali pawili kutoka kwenye Neno. Na hapo ni kutoka katika Isaya, mlango wa 53 wa Isaya. Ninataka kusoma kutoka kifungu cha kwanza—cha kwanza mpaka cha 10, hasa. Na halafu tunataka kusoma Mathayo 11:25 na 26. Sasa hebu na tusome.

Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Na mkono wa BWANA amefunuliwa nani?

Maana atakua mbele zake kama mche mwororo, na kutoka katika mzizi katika... nchi kavu; yeye hana umbo wala uzuri; na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani.

Anadharauliwa na kukataliwa na watu; mtu wa huzuni... ajuaye sikitiko;... kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.

Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu, na kuteswa.

Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa uovu wetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tunapona.

Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe;... BWANA... ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.

Alionewa, na kuteswa, aliteswa, na hakufunua kinywa chake; kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, na kama vile kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake; naam, hakufunua kinywa chake.

Kwa kuonewa na kuhukumikiwa aliondolewa; na maisha yake ni nani atakayeyasimulia? Maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu. Naye alikuwa yeye...

Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; na pamoja na matajiri katika kufa kwake; ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na wala hila kinywani mwake.

Lakini BWANA aliridhika kumchubua; amemhuzunisha; utakapofanya nafsi yake kuwa

dhahihu kwa dhambi, na ataona uzao wake, ataishi siku nyingi, na mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake;

55 Bila shaka, yeye anazungumza juu ya Yesu hapa, Bwana wetu mzuri sana na wa ajabu. Mathayo mlango wa 11, na ishirini- . . . vifungu vya 25 na 26.

Wakati ule Yesu akajibu, akasema, Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga.

Naam, Baba, hata . . .

Naam, Baba, kwa kuwa ndivyo ilivyopendeza mbele zako.

56 Sasa, Bwana akipenda, ninataka kutoa fungu la maneno kutoka kwenye haya, kuzungumza juu yake kwa kifupi tu, upesi niwezavyo. Kisha niketi chini kusikiliza shuhuda nyingine zaidi. Ninataka kuchukua somo hili hapa: *Mungu Akijificha Katika Urahisi.*

57 Mnajua, Mungu ni mkuu sana, Yeye hujificha katika urahisi, kisha anajifunua Mwenyewe katika jambo lile lile analojificha ndani yake. Naye Mungu ni mkuu sana, Yeye anaweza akajifanya wa kawaida. Hilo ndilo linalomfanya kuwa mkuu. Wengi sana wanamkosa katika urahisi, njia rahisi anazojifichia. Sasa, tunajua ya kwamba mwanadamu hawezi kufanya jambo hili. Mwanadamu hawezi kujifanya mkubwa vya kutosha kuwa rahisi. Unaona? Sasa kile kinachomfanya Mungu kuwa mkuu sana, ni kwa sababu Yeye anaweza kuwa wa kawaida sana. Wala Mungu hajifunui katika ukuu, ule tunaoita ukuu.

58 Sasa, tunapolisoma Neno, na kujifunza Neno la Mungu, tunaona jinsi Mungu anavyofanya mambo. Yeye hawezi, hawezi kamwe kubadilisha mpango Wake. Yale Mungu anayosema, Yeye hawezi kamwe kughairi Neno Lake.

59 Tunapofanya jambo lolote: ninaweza kufanya jambo fulani mwaka huu, ninafikiri, "*Hili ni sawa.*" Mwaka ujao ama labda juma lijalo, ninaweza kuona mahali nilipokosea.

60 Bali Mungu hawezi, kwa maana Yeye hana kikomo. Uamuzi Wake wa kwanza, kama Yeye atawahi kuitwa jukwaani, kutenda jambo, na jinsi anavyotenda juu ya uamuzi huo, hivyo ndivyo ambavyo hana budi kutenda kila wakati uamuzi huo unapopaswa kufanywa tena. Kwa maana, kama hakutenda hivyo; kama akitenda kwa namna fulani juu ya uamuzi *huu*, na jambo lilo hilo litokee tena, na kama Yeye hatendi vile vile alivyotenda mara ya kwanza, basi Yeye alikosea mara ya kwanza.

61 Kwa hiyo, kama mtu akija Kwake kwa ajili ya wokovu, Naye akamwokoia juu ya msingi aliomwokoia nao, hana budi

kumwokoza mtu mwingine juu ya msingi ule ule. Na kama mtu akija Kwake kwa ajili ya uponyaji, Naye amponye mtu huyo juu ya msingi fulani, kama mtu mwingine akija, Yeye hana budi kumponya juu ya msingi ule ule. Yeye hawezi kubadilika. Hana budi kudumu yeye yule.

⁶² Mungu alifanya mpango. Mwanadamu alipotenda dhambi hapo mwanzo, kule nyuma, alijaribu kujipatia njia yake mwenyewe ya kuepuka. Alijaribu kujifanyia kifuniko, majani ya mtini na kadhalika. Hakikufaa kitu. Bali Mungu alifanya njia ambayo mwanadamu angeweza kufanya ushirika pamoja Naye tena, na hiyo ilikuwa ni chini ya damu iliyomwagika ya kabadala kisicho na hatia. Na hiyo ndiyo njia pekee Mungu alivyowahi kukutana na mwanadamu. Na hiyo ndiyo njia pekee Mungu anaweza kukutana na mwanadamu, ni chini ya damu ya kabadala kisicho na hatia.

⁶³ Sasa, tuko hapa kwenye Ijumaa kuu. Na ulimwengu, leo, katika madhehebu ya Kikatoliki, wanatambaa kwenye vipandio, na, loo, njia nyingi sana mbalimbali ambazo tunafanya mapokeo, na kusugua mifupa. “Na kuna misumari kumi na tisa, iliyothibitishwa kabisa, misumari ambayo waliitoa kutoka katika mikono ya Yesu,” wao wanadai. “Kila kanisa lina mmoja.” Na inaleta tofauti gani kama ndio huo msumari, ama kama ni joho, ama chochote kile?

⁶⁴ Tuna Roho Mtakatifu. Huyo ndiye ambaye Kristo aliliachia Kanisa, si koti fulani, kipande fulani cha msalaba, msumari fulani, ama kitu fulani. Yeye alituachia kumbukumbu, na hilo lilikuwa ni Roho Mtakatifu ambaye alimwacha kwa ajili ya Kanisa. Sasa, sasa, huyo ndiye ambaye Yeye aliliachia Kanisa, miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, alasiri hii, alipokufa pale Kalvari. Aliikabidhi mikononi mwa—mwa Mungu Roho Yake, Nayo ikarudishwa kwa Kanisa kwenye Siku ya Pentekoste. Sasa, Mungu . . .

⁶⁵ Hapo mwanzo, wakati mwanadamu alipotenda dhambi, ilionyesha tabia ya mwanadamu. Yeye daima anajaribu kujificha kutoka kwa Mungu, na kujifanyia njia ambayo anaweza kujisikia amehesabiwa haki, dini fulani. Hiyo imekuwa ni *dini*, inayomaanisha “kifuniko.” Kwa hiyo alijaribu kutengeneza dini yake mwenyewe.

⁶⁶ Bali Mungu alifanya uamuzi Wake jinsi ambavyo angekutana na mwanadamu, huo ulikuwa ni juu ya Damu iliyomwagika. Na hiyo ndiyo njia pekee, haidhuru tunajaribu njia nyingine yoyote vipi. Hapo ndipo mahali pekee ambapo Mungu atakutana na mwanadamu kwa ajili ya ushirika, ni chini ya Damu iliyomwagika.

⁶⁷ Mungu alikutana tu na Israeli chini ya damu iliyomwagika. Mahali pekee ambapo Israeli wangeweza kuabudia ilikuwa ni chini ya damu iliyomwagika.

⁶⁸ Na, siku hizi, tumejaribu shirika, tumejaribu dhehebu, tumejaribu—tumejaribu elimu. Tumejaribu ufanisi wa kisayansi na kila kitu, kujaribu kumleta mwanadamu katika umoja wa ushirika. Na imeshindikana, kila moja ya hizo.

⁶⁹ Kuna mahali pamoja ambapo mwanadamu anaweza kukutana na kufanya ushirika pamoja na Mungu, na kufanya ushirika mmoja kwa mwingine. Hapo ni chini ya msalaba, wakati kila mtu anapokubali Damu ya Yesu Kristo. Sijali, katika upekee wake wote wa tabia, angali anaweza kunyosha na kuweka mkono wake kwenye mkono wa mtu huyo mwingine na kumwita “ndugu,” tunapokutana msalabani mahali Yesu alikufia.

⁷⁰ Tunabadilika kuwa watu wa wakati wa kisayansi. Kila kitu hakina budi kuthibitishwa, kisayansi. Tunaishi katika wakati wa sayansi, kama ilivyobashiriwa na Biblia, “wanyonge zaidi kuliko werevu,” kama tu- . . . kama ilivyobashiriwa. Nasi tunaishi katika wakati huo. Na kadiri tunavyozama zaidi katika sayansi, ndivyo tunavyoenda mbali na Mungu. Kamwe hutaweza kumthibitisha Mungu kisayansi.

⁷¹ Na silaha zote za Mkristo ni za rohoni kabisa. Hakuna kitu cha maumbile ya kawaida. Kama unaweza kumthibitisha Mungu, basi hakuna tena haja ya imani. “Bali yeye amjiaye Mungu hana budi kuamini ya kwamba Yeye yuko.” Ni kwa imani. Silaha zote za Mkristo ni imani.

⁷² Dkt. F.F. Bosworth, mmoja wa mameneja wangu wa hapo awali, aliandika kitabu kiitwacho *Kuangalia Yasiyoonekana*. Sasa, wengi wenu mmekisoma, hapana shaka. Ni kitabu kizuri sana, ninii. . . cha kuangalia yasiyoonekana. Mkristo huangalia mambo asiyoyaona.

⁷³ Sasa hebu na tuangalie silaha za Ukristo tuone kama ni za rohoni: upendo, furaha, amani, imani, uvumilivu, upole, utu wema, subira. Kila kitu ni cha rohoni. Upendo! “Shuka uende kwenye duka la madawa ukaninunulie upendo wa shilingi ishirini na tano. Ninauhitaji.” Unaona? Usingeweza kufanya jambo hilo. Hebu ninunulie amani yenye thamani ya dola moja. Usingeweza kufanya hilo. Unaona? Kila kitu ni cha rohoni. Silaha zote za Mungu ni za rohoni. Kanisa Lake ni la kiroho. Si dhehebu. Ni Mwili wa kimbinguni ambamo wanaume na wanawake wanazaliwa na Roho Mtakatifu, na njia Yake rahisi.

⁷⁴ Mungu hafanyi mambo kuwa magumu, ya rozari kadhaa, na vitu vingi *hivi*, na kujiunga na *hili*, na elimu kubwa mno, thiolojia kubwa mno. Mbona, tunazidi kujipeleka mbali zaidi na zaidi na Mungu, wakati wote, kwa kufanya hivyo.

⁷⁵ Leo, sisi ni wa kisayansi sana hata tunaweza kusema inachukua molekuli ngapi kufanya atomu moja, ni elektroni ngapi, na kadhalika; na kuipasua hiyo atomu, na kuwaambia jinsi ya kufanya hivyo; kuunda bomu la atomiki, na halafu

tungeweza kuelezea jinsi tulivyolitengeneza; lakini tunatembea juu ya jani la nyasi ambalo hatuwezi kulielezea.

⁷⁶ Mungu, katika urahisi. Mungu alijidhihirisha katika urahisi. Yeye hujifanya wa kawaida. Ni kusudi kwamba wenye hekima wasifahamu. Yesu alisema, “Nakushukuru, Baba, umeficha jambo Hili wenye hekima na akili, na utalifunua kwa watoto wachanga ambao watajifunza.”

⁷⁷ Kamwe usijaribu kujielimisha umfahamu Mungu. Unapofanya hivyo, unajielimisha kwenda mbali na Mungu. Unaona? Mungu hajulikani kwa elimu. Mungu, ni wa kujulikana kwa imani. Na pigo la kwanza ambalo Ibilisi alipiga nalo lilikuwa ni kwenye mpango wa elimu, ndipo mwanadamu akapoteza ushirika wake na Mungu. Hiyo ni kweli kabisa. Hana budi kumjua Mungu kwa imani, si yale anayoweza kuelezea; kwa yale anayoamini, ambayo hawezi kuelezea. Ni kwamba, tunabadilisha tu picha hiyo.

⁷⁸ Sasa, siku hizi, kila kitu ni mradi wa elimu. Naam. Tunatembea juu ya jani dogo la kawaida la nyasi. Tunawapeleka watoto wetu kwenye shule za Biblia na vyuoni. Sasa, kumbukeni, sipigi marufuku jambo hilo. Siungi mkono ujinga. Bali ninajaribu kuwaambia upuuzi wake. Na hapo ndipo tunapofanya . . . Unajua kuna kasoro fulani.

⁷⁹ Na ni kama vile katika mikutano yangu. Karibu wakati wote, ninapokuwa na mikutano, ninapata wale wanaoshindikana kwenye mikutano ya wengine. Kwa sababu, mara nyingi . . .

⁸⁰ Nimemwanguka Ndugu Roberts. Mtu fulani alisema, “Ndugu Roberts, Ndugu Branham, ataombea mia tano wakati wewe unaombea watatu.” Hiyo ni kweli. Hakika. “Yeye atapokea shuhuda maradufu.” Hakika. “Mara hamsini ya shuhuda.” Unaona? Kwa maana utaninii . . . Hata hivyo, msingi wake ni juu ya imani ya watu binafsi wanaoombewa. Lakini, wale wanaoshindikana kule, basi wao huja kwenye mkutano. Kwa sababu . . .

⁸¹ Hapa, huyu hapa daktari ameketi. Kama daktari . . . Ukienda kwenye ofisi ya daktari, useme, “Mimi ninaumwa na tumbo, na ninaumwa na kichwa, na kadhalika.” Na daktari huyo anakuandikia tu maagizo mafupi ya matumizi ya—ya aspirini ama dawa ya kutuliza maumivi, kitu fulani, yeye hajachunguza na kubainisha ugonjwa huo. Yeye anajaribu tu kukuondoa ofisini mwake. Unaona? Sasa, kama yeye anakuthamini, na kukusikitikia, atachunguza na kubainisha ugonjwa huo mpaka atakapopata chanzo chake.

⁸² Na wakati mwanamume fulani ni mgonjwa, ama mwanamke, na jambo fulani limetukia, kuna njia moja tu ya kupata jambo hilo sahihi, hiyo ni, rudi nyuma na utafute chanzo chake. Turudi nyuma mpaka tutakapoona yale waliyofanya. Katika mikutano, waangalie wakisimama pale jukwaani. Roho

Mtakatifu atasema, “Miaka kumi iliyopita, ulikuwa mahali *fulani*, na ulifanya jambo *fulani*. Na ulifanya *hivi*, na ninii *fulani*.” Mmesikia jambo hilo, wengi wenu, mikutanoni. Unaona? “Ulifanya hivyo. Huna budi kusahihisha jambo hilo, kwanza.” Na basi, kama wakiahidi kufanya jambo hilo, basi mtasikia likija, “BWANA ASEMA HIVI.” Liandikeni kwenye vitabu vyenu. Je! mliwahi kuliona likishindwa? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] La, hashu. Halishindwi. Haliwezi kushindwa. Ni kitu gani? Unaona? Wewe, jambo la kwanza, huna budi kupata chanzo chake kabla hujapata tiba yake. Inakubidi kupata sababu ya jambo hilo.

⁸³ Na sasa, leo, tunajaribu kuwaelimisha watu katika mambo hayo, kumwendea Mungu kisayansi, na huwezi kufanya hivyo. Mungu hajulikani kwa sayansi, bali kwa imani tunamjua Mungu.

⁸⁴ Nami ningesema hivi, ya kwamba—ya kwamba mtu anaweza kuketi chini na kuangalia tawi la maua, shada la maua, na kulisoma hilo kwa dakika thelathini, kwa uaminifu kwa moyo wake wote, na ajue zaidi juu ya Mungu kuliko ambavyo angejua, kama angelikuwa na digrii ambazo shule ya Biblia ingaliweza kumpa, kwa maana Mungu hujifunua katika ua. Tunaliona likifa na kufufuka tena, ufufuo. Tunaona rangi mbili ama tatu katika aina ile ile ya ua. Hiyo rangi ilitoka wapi? Nielezee jambo hilo. Ilifikaje pale? Inaenda wapi, na inarudi tena namna gani? Hiyo mbegu inapaswaje kufa, na kuoza, na kurudi tena? Mungu, akijionyesha katika urahisi, kisha akijificha tena katika mauti, apate kujionyesha tena katika ufufuo. Unaona? Ni ninii tu. . .

⁸⁵ Si lazima ujue chungu nzima ya mambo. Jambo pekee linalokupasa kujua ni kuwa na imani katika yale unayoangalia, yale unayoamini. Unaona? Amini. Saa moja ingethibitisha jambo hilo kweli kweli, ingekufundisha mengi zaidi juu ya Mungu kuliko digrii zote ambazo ungeweza kupata.

⁸⁶ Mungu ni mkuu sana, Yeye anaweza kujifanya rahisi. Sasa, hilo ndilo linalomfanya Mungu kuwa mkuu, kwangu mimi, ni jinsi anavyoweza kujifanya rahisi. Na hilo, kwa kujifanya, Mwenyewe, Yeye hujificha kwa wenye akili na hekima. Sasa hebu wazia tu juu ya jambo hilo. Yeye hujificha kwa watu wenye akili na kujifunua kwa watu wanyenyekevu. Biblia ilisema, katika Isaya 35, “Hata, ajapokuwa mjinga hatapotea katika njia hiyo, Hiyo ni njia rahisi sana.” Na kadiri unavyojaribu kuielewa, na kuisoma, utamfahamu tu Mungu vibaya. Kila wakati unapofanya hivyo, ndivyo unavyozidi kujipeleka mbali zaidi na zaidi. Acha kujaribu kuelewa jambo Hilo. Amini tu alilosema. Hakuna lingine, liamini tu. Na kisha anajificha kutoka kwa wenye hekima, na kujionyesha kwa watu wa kawaida. Mwanadamu hawezi kuwa mkubwa namna hiyo.

⁸⁷ Mwanadamu, mara tu anapojipatia digrii ya namna fulani, yeye anajua mengi zaidi kuliko jamaa huyo mwingine. Huwezi kumwambia chochote. Mekanisa, siku hizi, yanapenda kujivunia mchungaji wao, kwa maana yeye ni mwanafunzi wa seminari *fulani*. Yeye a—ana B.A., ana D.D., L.D. Vema, hilo halimaanishi kitu. Hilo halina maana. Huenda akawa na B.A., na D.D., na L maradufu, na D., na hata asiweze kutofautisha kati ya njegere zilizopasuliwa na kahawa. Hilo—hilo halimaanishi... Samahani kwa tamshi hilo. Hapa si mahali pa utani, unaona. Si—simaanishi jambo hilo. La, bwana. Samahani. Ninamaanisha hivi, ya kwamba hilo halina uhusiano wowote Nalo.

⁸⁸ Unamjua Mungu kwa imani, na ni hiyo pekee. Hilo lilithibitishwa wakati Yesu alipokuja duniani, na wale Mafarisayo na kadhalika, watu wenye digrii za hali ya juu sana, werevu sana, watu wanaoishi kitakatifu sana tuliopata kuwa nao. Wakiwa tu na hitilafu moja tu dhidi yao, wangepigwa mawe bila huruma. Na Yesu alisema, “Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi; kazi zake mtazifanya.” Ni nani angeweza kuwaelekezea kidole na kusema?

⁸⁹ Tunaita, “dhambi,” kufanya uzinzi, kusema uongo, kuvuta sigara, kutafuna tumbaku. Ninii...Hiyo si dhambi. Hayo hayana uhusiano wowote na dhambi. Hayo ni matokeo ya kutokuamini. Kuna dhambi moja tu, hiyo ni kutokuamini. “Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari.” Wakati mtu anapokana jambo Hilo, Hilo, Neno la Mungu, hiyo ndiyo dhambi papo hapo.

⁹⁰ Yesu alisema, wakati alipokuwa duniani, “Ni nani anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi? Ni nani anayeweza kunionyesha ya kwamba sikutimiza yote yaliyotabiriwa juu yangu? Nilipokuja, nilipaswa kufanya mambo *kadha* na *kadha*. Ni nani anayeweza kuthibitisha ya kwamba sikufanya vile hasa Maandiko yanavyosema nifanye? Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Uaona? “Ni nani anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi?”

⁹¹ Sasa, hao watu pale, loo, ilibidi kuosha vyungu vyao na mabirika, na kunawa kabla ya kula, na mapokeo haya yote ya kila siku waliyopaswa kupitia. Lakini Yesu aliyakataa yote, na kuyaweka kando, na kuwaambia wao walikuwa ni pepo. Ungeweza kuwazia jambo kama hilo?

⁹² Je! unaamini Yeye angefanya jambo lilo hilo makanisani leo? Bila shaka angefanya hivyo. Tumejisokota kwenye mapokeo na kadhalika, mpaka tukajiingiza katika mchafuko ule ule tulimokuwa wakati huo. Na sasa, wakati Mungu anapojionyesha katika urahisi, ndipo wao hawatambui jambo Hilo, hata kidogo. Limepita fahamu zao. Wamelipangia jinsi wanavyofikiria kwamba linapaswa kuwa, na, kama haliji namna hiyo,

hawatalipokea. Hiyo ndiyo njia pekee. Hiyo ndiyo iliyokuwa shida sikuzote.

⁹³ Kumbukeni, njia ya kupanda juu ni kushuka. Sasa, hiyo ni kweli. “Yeye ajidhiliye atakwezwa.”

⁹⁴ Unajuaje kama ndivyo ilivyo, wapi ni juu, na wapi ni chini? Kama ulimwengu unasimama angani, je! Ncha ya Kaskazini ni juu, ama Ncha ya Kusini ndiyo iko juu? Ni ipi? Unaona?

⁹⁵ Nawe unasema, “Loo, nyota ya asubuhi, na nyota ya jioni.” Zote mbili ni nyota ile ile. Unaona? Nuru ile ile iliyoangaza asubuhi, ndiyo nyota ile ile ya jioni, ulimwengu umezunguka tu. Basi. Unaona? Kwa hiyo si jambo gumu sana, hata hivyo. Ni imani rahisi tu, kumwamini Mungu. Angalia. Njia ya kwenda juu, nilisema, ni kushuka. Yeye. . .

⁹⁶ Inatupasa kumwamini Mungu. Inatupasa kumchukua katika Neno Lake. Haitupasi kuwazia mambo. Lakini, lolote tu Mungu analosema, Roho halisi wa Mungu ataitikia kila Neno la Mungu kwa “amina.” Roho Mtakatifu aliandika Neno.

⁹⁷ Kama Roho Mtakatifu ndiye aliyeandika Neno, na Roho Mtakatifu yumo ndani yako, anawezaje kusema, “Vema. Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine”? Anawezaje kusema, wakati liliposema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” na unajaribu kuliweka katika wakati fulani kule nyuma, ama wakati fulani ujao?

⁹⁸ Mwanadamu angali ni yeye yule. Daima anamshukuru Mungu kwa yale aliyofanya, akitazamia mbele kwa yale atakayofanya, huku anapuuza yale ambayo Yeye anafanya. Hivyo ndivyo binadamu alivyo hasa, sikuzote. Naye anafanya jambo lile lile siku hizi. Yuko hivyo daima. Yeye, huyo ni mwanadamu, nawe inakupasa kutoka katika hilo. Inakupasa kuruhusu nia iliyokuwa katika Kristo iwe ndani yako.

⁹⁹ Mungu anaposhughulika na mwanadamu imekuwa daima ni katika unyenyekevu. Yeye kamwe hashughuliki na wanadamu katika masharti makubwa mno ya kiteolojia. Niambie wakati mmoja alipowahi kufanya jambo hilo. Kamwe hafanyi hivyo. Yeye anajifanya rahisi. Na mwanadamu anataka kulifanya gumu. Yeye hujifanya mkubwa, kwa kujinyenyekeza.

¹⁰⁰ Sasa, mtu anapopata elimu kidogo, ama digrii chache, yeye anajua mengi sana mpaka huwezi kumwambia kitu. Lakini kama angeliendelea tu kuwa mkubwa vya kutosha mpaka angeweza kujifanya kuwa mdogo, mpaka awe hajui kitu, basi ingekuwa ni sawa. Lakini yeye hawezi kuwa mkubwa namna hiyo. Unaona? Yeye hawezi kuwa mkubwa namna hiyo.

¹⁰¹ Basi Mungu ni mkubwa hivyo. Yeye ni mkubwa sana mpaka anaweza kujinyenyekeza. Bali sisi hatuwezi, wakubwa, kuwa wakubwa vya kutosha kujinyenyekeza. Hiyo ndiyo tofauti. Na kwa hiyo Mungu hujificha katika unyenyekevu na urahisi.

Na mwanadamu, hekima ya ulimwengu, inatazama kuvuka moja kwa moja jambo Hilo. Si ajabu Isaya alisema, “Ni nani aliyeamini habari tuliyoleta? Mkono wa Bwana amefunuliwa nani?” Yesu alisema, “Ninakushukuru Baba, wa Mbinguni, wa dunia, ya kwamba umeficha jambo Hili kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili, na utalifunulia watoto wachanga walio tayari kujifunza.” Unyenyekevu, urahisi, angalia tu jinsi Mungu anavyojifanya Mwenyewe kuwa rahisi.

¹⁰² Angalia. Angalia Edeni. Liamini tu Neno Lake, ndivyo tu walivyopaswa kufanya, wapate kuishi. Sasa, Mungu kamwe hakusema, kwa kipindi hiki cha mwanzo, ya kwamba una digrii kadhaa za chuoni unazopaswa kupata. Yeye alisema, “Hili ni Neno Langu. Liamini, uishi. Likatae, ufe.”

¹⁰³ Sasa, Hawa kamwe hakulikataa lote. Aliamini tu sehemu Yake moja ndogo.

¹⁰⁴ Sasa nataka kuwauliza swali, ndugu, dada. Kama Mungu aliacha haya yote yatukie kwa sababu Hawa alikosa kuamini sehemu moja ndogo ya Neno, na kusababisha wanadamu kufikia mahali walipo, je! mnafikiri kamwe tutarudi, tusipoamini sehemu yoyote Yake? Wazia jambo hilo. Kama Mungu angeweza kuona watoto wachanga wakiteseka, vita na shida, njaa na kukosa chakula, magonjwa na mauaji na mambo haya yote ambayo yametukia, yote kwa sababu sehemu moja ndogo ya Neno Lake ilitiliwa shaka. Je! unafikiri tutarudi, tukitilia shaka sehemu Yake moja? Kama iligharimu yote haya, je! Yeye atakuruhusu urudi bure, akuache uende mahali popote, useme, “Sijali. Siwezi kufahamu jambo Hilo. Siliamini, kwa vyovyote vile”? La.

¹⁰⁵ Inakupasa kuliamini lote, haidhuru linaonekana ni dogo namna gani. Liamini, hata hivyo. Unasema, “Kabisa, silielewi Hilo.” Liamini, kwa vyovyote vile. Haikupasi kulielewa. Unapaswa kuliamini. Liamini tu, hata hivyo. Sasa, hivyo ndivyo tulivyo siku hizi, jambo lile lile, huyo ni Mungu.

¹⁰⁶ Ni kama tu vile jeshi linapoenda vitani. Tuna wapelelezi huko Uingereza. Uingereza ina wapelelezi hapa. Wapelelezi wanaingia na kutoka, kote ulimwenguni. Kwa nini? Wanatafuta kujua siri zetu za kijeshi. Tunapopata siri fulani ya kijeshi mara tu wanapoweza kuzipata, wanachukua jambo lilo hilo, ama chochote kile, kupigana nacho. Ni vita.

Vita vikali sana, vinavyoendelea, ni vita vya kiroho.

¹⁰⁷ Sasa, wakati Mungu alipojua jambo hili litakuja kutukia, Yeye aliwafanyia watoto Wake jinsi tu Marekani inavyolifanyia jeshi lao. Tunampa mtu helmeti ya kuvaa, kwa maana tunajua ataitumia. Tunampa se—sepeto ya kuchimbua. Tunajua ni uzani mkubwa, mzigo wa karibu ratili tisini mgongoni mwake. Maskini askari kurutu anaubeba, bila shaka ni kitu ki—kigumu kwake. Lakini jeshi linajua halina budi kumpa mazoezi kwa ajili

ya hivyo, kwa sababu atavihitaji. Kila kifaa, yeye atakihitaji atakapofika vitani.

¹⁰⁸ Na hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya siku hizi, rafiki. Inatupasa kuchukua Neno lote la Mungu, maana tutalihitaji. Hatuna budi kutumia kila Neno lililo Mle. Ni BWANA ASEMA HIVI, na inatubidi kutumia Injili yote, yote Hiyo. Sasa, wakati Mungu alipolikinga Kanisa Lake, Yeye alilikinga kwa kitu kizuri sana ambacho angeweza kupata, kwa maana ni watoto Wake Mwenyewe. Naye alilikinga Kanisa kwa Neno, Neno Lake Mwenyewe. Kuwaambia waliamini tu Neno Lake, ni hayo tu basi.

¹⁰⁹ Na Shetani, kwa hekima yake, alimfanya Hawa avunje kizuizi hicho, mahali fulani tu. Shetani alikubali kila sehemu ya hilo Neno ilikuwa ni kweli, lakini akasema, “Hakika...” Hiyo ndiyo aliyopaswa kujua. “Hakika hamtakufa” Sasa, huo ndio uliokuwa ule mwanya. Alimtoa Hawa nyuma ya Neno hilo, kwa shaka moja ndogo.

¹¹⁰ Hapo ndipo mahali hasa anapolipata kanisa siku hizi, jambo lile lile. Hiyo shaka moja ndogo tu inakuleta upande huu. Na sasa kamwe hakuna njia ya kufikiria ya kwamba kuna wakati Mungu atakuhurumia kwa kuwa mfuasi wa kanisa fulani, kuwa mfuasi wa shirika fulani, ama kundi fulani, ama chochote kile, ama kwa mhemuko wowote.

¹¹¹ Huna budi kuamini Neno Lake na kulitekeleza jinsi lilivyo. Kweli. Kuna... Hiyo ndiyo njia pekee. Huo ndio mpango wa Mungu hapo mwanzo. Huo ndio mpango wa Mungu kote katika maisha. Huo ndio mpango wa Mungu sasa, ni, Kanisa halina budi kukaa nyuma ya Neno. Hiyo ndiyo njia pekee ambayo yeye, unayoweza kuwa salama.

¹¹² Angalia Nuhu katika siku zake. Tulinena habari hizo asubuhi ya leo. Katika siku zake ulikuwa ni wakati mkuu wa elimu, na watu walikuwa werevu. Na Nuhu, wakati wake mkuu wa kiakili, Mungu alishuka akaja kuwaokoa watu walioteuliwa.

¹¹³ Je! unaamini Mungu ana kanisa lililoteuliwa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Bila shaka, Yeye analo. Naye anakuja kuwaokoa hao Wateule. Hao wengine, ni takataka za kawaida za kuteketezwa. Lakini Yeye—lakini Yeye anajua kwamba kutakuwa na idadi fulani ya wale watakaookolewa, kwa sababu, “Yeye aliweka majina yao katika kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Hilo ni kulingana na Maandiko kabisa.

¹¹⁴ “Na mpinga-Kristo, siku za mwisho, atamdanganya kila mmoja ambaye majina yao hayakuandikwa katika kitabu hicho kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Biblia ilisema hivyo. Mpinga-Kristo, yuko karibu sana, itakuwa ni Pentekoste, juu ya alama. Unaona? “Bali itawapoteza hao ambao majina

yao hayakuandikwa katika Kitabu cha uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa.”

¹¹⁵ Angalia. Sasa, tunaona ya kwamba, Shetani, yule mtekelezaji mkuu, yeye aliweza tu kulipata kanisa, mara ya kwanza, kwa kuwafanya wakubali hekima yake ya ulimwengu, na kuiacha imani ya pamoja ya watu wote ambayo Mungu aliwaambia kuwa nayo katika Neno Lake. Huo ulikuwa ndio mpango wake wa kwanza. Alifanikiwa hapo. Na hapo ndipo alipofanikiwa, kila wakati. Loo, laiti tungaliweza kuona ya kwamba hilo ndilo jambo lenyewe. Na wakati anapoweza kukuondoa kutoka nyuma ya Neno hilo, hivyo tu ndivyo inavyompasa kufanya. Uko—uko mikononi mwake papo hapo.

Angalia, amini tu Neno Lake, na uishi.

¹¹⁶ Sasa, Hawa, Hilo halikumtosha. Ilimbidi apate hekima fulani ya ulimwengu.

¹¹⁷ Hivyo ndivyo tunavyofanya siku hizi. Inatubidi tu kumpata daktari fulani, Ph.D, LLD., kutuambia habari Zake. Ndugu, kama ni kinyume cha Neno hili, liache. Sijali kama ni papa wa Rumi, ama kama ni ninii... ukasisi wowote, ama askofu mkuu wa Canterbury. Sijali ni nani. Wewe amini Neno la Mungu. Na acha neno lingine lolote liwe ni uongo, kama chochote ni kinyume cha Neno.

¹¹⁸ Nimegundua jambo hili moja. Ishi kwa Neno. Kama Mungu akifanya ahadi, Yeye hana budi kutimiza Neno hilo. Kama hatimizi Neno hilo, basi si Mungu.

¹¹⁹ Sasa, Mungu yuaenda kuuhukumu ulimwengu kwa kipimo fulani, siku moja. Sasa, kama Yeye atauhukumu kwa kipimo kama vile kanisa la Kirumi linavyotwambia, cha kanisa, basi ni kanisa lipi? Kuna madhehebu mia tisa mbalimbali. Ni lipi? La Kibaptisti linasema lao ndilo kipimo, la Kipentekoste linasema ni lao. La Katoliki linasema ni lao. Kwangu mimi, si hata moja lao.

¹²⁰ Neno ndiyo Kweli. “Kila atakayeondoa Neno moja kutoka kwa Hili, ama kuongeza neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa kwenye Kitabu cha Uzima.” Unaona? Ni Neno la Mungu, ndilo Mungu atakalomhukumu mwanadamu kwalo.

¹²¹ Kizazi mashuhuri cha Nuhu pale, wakati wao walipokuwa werevu sana, Mungu aliwatumia ujumbe. Na wakati alipowatumia, Yeye kamwe hakumtuma malaika fulani mkuu. Alimtuma mkulima, akiwa na ujumbe mdogo, rahisi, bali ulikuwa ukiwaonyesha. Asa, unafikiri wanaupokea? La. Kwa sababu, ulikuwa rahisi mno. Kama—kama haungekuwa rahisi sana, wangeupokea. Kama ungelikuwa kitu fulani kikuu, ungeweza kuwaambia jinsi ya kujenga piramidi iliyokuwa kubwa zaidi ya zile nyingine walizokuwa tayari wamejenga, na kadhalika, huenda wangaliupokea. Lakini Yeye alimtuma mtu wa kawaida akiwa na ujumbe, ya kwamba, “itanyesha.”

Huo haukuridhisha elimu yao ya kisayansi. Mbona, waliweza kurusha angani, kwa rada ama kitu fulani, na kuthibitisha hakuna maji kule.

¹²² Lakini Nuhu alisema, “Mungu alisema kutakuwa na maji kule. Na kama Mungu alisema kutakuwa na maji kule, ingawa hakuna yoyote kule, Yeye anaweza kuyaweka kule, kwa maana Yeye ni Muumba.” Hivyo ndivyo ilivyo. Haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini, Mungu alisema hivyo, na Mungu anaweza kutimiza Neno Lake. Ujumbe huo mdogo, rahisi, uliuhukumu ulimwengu katika siku zake, na kuiokoa nyumba yake mwenyewe. Hiyo ni kweli. Juu ya jambo rahisi, si la kimapinduzi, lilikuwa tu, kwa urahisi, ni “Ingia katika safina.” Hayo tu ndiyo yaliyohitajika. “Amini na uingie.” Mungu aliukoa ulimwengu kwa urahisi, akijionyesha Mwenywe kuwa mnyenyekevu sana. Hiyo ilikuwa. . . Ilikuwa ni kitu gani? Mungu akijificha tena kutoka kwa walio werevu kweli kweli, wenye elimu.

¹²³ Mtu yeyote anajua ya kwamba watu wa zama zilizotangulia ile gharika walikuwa werevu kuliko tulivyo leo, waliendelea zaidi katika sayansi, na kadhalika, kuliko tulivyo siku hizi. Mbona, wanaweza kuchimbua mumiani kule nyuma. Na sisi tusingeweza kuwa na mumiani leo. Tusingeweza kuukausha mwili namna hiyo. Walikuwa na rangi tuzizoweza kuzilinganisha na za siku hizi. Walijenga mapiramidi na sfinksi, na kadhalika, ambayo tusingeweza kujenga hata tukifanya nini. Hatuna vifaa vya kuzijengea. Hatuna nguvu za kuziinua kule juu. Tusingweza kuijenga, bali wao waliijenga. Kwa nini? Wao walikuwa ni werevu kuliko tulivyo sisi.

¹²⁴ Na katika jamii hiyo nzuri ya watu, wenye elimu, werevu na wenye akili, Mungu alituma Ujumbe, mnyenyekevu sana, ambao uliwakwaza kabisa kabisa. Wao—wao waliupuuza na kuukataa. Na haki ya Mungu ilihitaji hukumu, wale walioukataa ujumbe Wake, na Yeye aliuhukumu ulimwengu na kuuzamisha chini ya ardhi, kwa gharika. Kisha akamwokoa Nuhu, mwenye haki, ambaye aliamini kwa ujumbe mdogo, rahisi ambao Mungu aliutumia. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu akijificha katika urahisi. Loo, naam. Naam, bwana. Kwa kawaida, kama wanavyofanya sikuzote, waliuamini.

¹²⁵ Wakati mwingine, wakati ukombozi ulipokaribia, Mungu alimtuma mtu wa kawaida, kutoka kwenye familia ya kawaida. Yeye kamwe hakuchukua familia iliyotukuka. Familia ya Musa, tunaona ya kwamba yeye alikuwa tu ni mtu wa kawaida, familia ya kawaida ya kabila la Lawi, ninaamini. Nao wakawatoa, familia hii.

¹²⁶ Alimwachilia Musa aingie na awe mtu mwenye elimu sana kuliko wote kote nchini. Angeweza kuwafundisha Wamisri hekima. Alikuwa mwanajeshi, tunaambiwa na historia. Yeye

alijua mambo yote kwa ndani na nje, jinsi ya kufanya mambo. Naye Mungu akamwacha afunzwe namna hiyo, na akathibitishe ya kwamba huwezi kufanikisha mambo kwa ajili ya Mungu hivyo. Kipaji chake cha kijeshi, elimu yake yote, yeye alishindwa vibaya sana kwayo. Mungu alimwacha afanye jambo hilo, alimwacha apate elimu na awe mwerevu. Ndipo basi ikamchukua miaka arobaini kumpa mafunzo, na halafu miaka arobaini kuiondoa kwake, kabla Yeye hajaweza kumtumia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Alimchukua akampeleka huko ndani ndani kabisa ya jangwa na kuitoa elimu yote aliyokuwa nayo.

¹²⁷ Loo, shida tu iliyopo leo, daima tunajaribu tu kujaza mambo, kwa ajili ya kule kuja. Tunapaswa kuwa tukiya mwaga tuwe tupu, kwa ajili ya kule Kuja. Inapasa kuwe na nafasi pale. Kunapaswa kuwe na kitu fulani, njaa fulani. Tunajaribu kushawishi na kuvuta. Haitupasi kufanya hivyo. Kama mtu ana njaa ya Mungu, kuna mahali patupu, kwa ajili Yake. Hivyo tu. Lakini, mpaka mahali hapo, hatuwezi kumkandamiza Mungu mahali fulani. Huenda tukamfanya awe na itikadi, na mizizimo, na kudhalika, na kutenda kiajabuajabu. Lakini kwa hakika hayo hayatafanikiwa mpaka mtu huyo, mwenyewe, awe anamtaka Mungu. Naam, bwana. Kwa hiyo mipango yetu ya kujibunia haifai kitu. Ingia ndani ya ule wa Mungu. Hiyo ni kweli kabisa. Kujiunga na kanisa, kupeana mikono, aina mbalimbali za ubatizo, na matambiko, na—na rozari, na kadhalika, upuuzi!

¹²⁸ Ni kuzaliwa. Na Mungu... “Heri wenye njaa na kiu ya haki, kwa maana atajazwa.” Hiyo ni kweli. Huna budi kuwa na sehemu tupu. Ni kitu gani kinachowafanya watu kuona njaa?

¹²⁹ Ni kitu gani kinachowafanya watu watoke hapa nje na kufanya vile wafanyavyo? Ni kitu gani kinachowafanya hawa wanawake huko mtaani, watembee wamevaa nguo hizi mbaya? Wanajaribu kufanya nini? Wanajaribu kuridhisha njaa fulani. Nao wanaona njaa ya kitu gani? Ni kwa sababu waliumbwa wapate kuona njaa. Lakini njaa hiyo, mtu yeyote anathubutuje kutuliza hiyo njaa takatifu, ambayo Mungu alikufanya, kumwonea njaa, na kujaribu kuiridhisha kwa mambo ya dunia. Huna haki ya kufanya jambo hilo.

¹³⁰ Mtu yeyote anathubutuje kujaribu kuweka michezo ya kamari na madansi na upuuzi kanisani, na karamu za supu kwa ajili ya kumlipa mchungaji wenu, namna fulani ya kujiburudisha kimwili, na kujiita kwamba ni tu wa dini, na vitu kama hivyo, kutuliza hiyo njaa takatifu! Wakati, mnapaswa kuwa na chumba cha juu kule, mkiomba kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu kwamba ulijaze kusanyiko hilo la watu. Hamna haki.

¹³¹ Lakini ni jambo nyenyekevu mno. Halitoshelezi matakwa yenu. Elimu yenu imevuka huo. Unaona? Ninyi ni werevu sana. Mnataka kuwaelimisha watu kuingia. Hamtaki mchungaji anayemjua Roho Mtakatifu. Mngemfukuza atoke mimbarani

mweni. Hamtaki jambo hilo, kwa maana hawezi kuonyesha kadi yake. Hawezi kuonyesha alitokea shule gani. Mnafikiri Musa angeweza kuionyesha? Mnafikiri yeyote wa hao manabii angeweza kuonyesha? Je! Yesu angaliionyesha?

¹³² Walisema, “Unatokea shule gani? Yeye alipata elimu hii wapi? Hii ilitoka wapi?” Hatuna kumbukumbu Yake kwamba alienda shuleni hata siku moja maishani Mwake.

¹³³ Vipi kuhusu Yohana, yule mzee mwenye uso uliojaa mvi, na ndevu za kipilipili, akitokea huko nyikani namna hiyo? Baba yake alikuwa mhubiri, na alitoka kwenye shule fulani; alikuwa kuhani. Hata hatuna kumbukumbu yake yoyote kwamba aliwahi kwenda shuleni. Alienda jangwani akiwa na umri wa miaka tisa. Kwa nini? Alikuwa na kazi muhimu ya kufanya. Kwa nini hakufuata nyayo za baba yake, kama tu ilivyokuwa desturi kwa yeye kufanya? Mbona, hiyo seminari huko chini inge—ingemwingiza katika vurugu nyingi sana walizokuwa nazo, “Sasa, unajua unapaswa kumtangaza Masihi. Sasa, unajua Ndugu Jones ndiye anayefaa kwa jukumu hilo.”

¹³⁴ Alitoka akaenda nyikani akamngojea Mungu mpaka Bwana akamwambia, “Yeye Ambaye utaona Roho akishuka na kukaa juu Yake, Yeye Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.” Huduma yake ilikuwa muhimu sana hata hakuhitaji kupata elimu. Bila shaka ilikuwa muhimu. Ilimbidi apate nguvu za Mungu.

¹³⁵ Sasa, kama una elimu yako pamoja na nguvu za Mungu, ni vizuri sana, bali usiweke elimu hiyo juu ya nguvu za Mungu. Unaona? Hakika.

¹³⁶ Sasa, tunaona ya kwamba Musa, sasa, wakati alipokuwa huko nje, yeye... Alijifunza kwa muda wa miaka arobaini, akijua kutokana na mama yake ya kwamba alikuwa awakomboa wana wa Israeli. Akadhania kwa hakika, wakati alipomwua yule Mmisri, ya kwamba wale ndugu wangelielewa jambo hilo, bali hawakulielewa. Kwa hiyo, kwa mbinu zake zote, alishindwa tena alishindwa vibaya sana. Lakini katika dakika tano, hapo Uweponi mwa kijiti kilichowaka moto huko mbali, Mungu aliingiza mengi zaidi ndani yake kuliko se—seminari ilivyomwingizia kule chini katika muda wa miaka arobaini.

¹³⁷ Sasa, nitakubali jambo moja, unapojifunza Mungu, ya Mungu, katika unyenyekevu. Na kijiti je? Vipi kama Musa angesema, “Sasa, ngoja kidogo. Elimu yangu ni ya juu sana. Kwa hiyo nafikiri nitaenda kule na kujaribu kuokota baadhi ya yale majani machache kutoka katika kile kijiti, niyapeleke kwenye maabara, na kuyachunguza, nione ni kemikali gani ambayo hayo yamepuliziwa, nione kama ninii... kinawaka moto na hakiungui”? Unaona, yeye kamwe asingepata hiyo siri. Bali yeye alienda mpaka kwa Mama Maumbile, akavua viatu vyake,

akapiga magoti na kuanza kuzungumza Nayo. Nayo ikamjibu. Hivyo ndivyo mtu unavyopaswa kufanya.

¹³⁸ Usijaribu kufahamu jambo kwa kulingilia kielimu. Lakini nenda magotini moja kwa moja mbele za Yehova Mungu, zungumza Naye, Yeye atakujibu tena. Hivyo ndivyo jambo hilo lilivyo nyenyekevu. “Ombeni, nanyi mtapata. Bisheni, nanyi mtafunguliwa. Tafuteni, nanyi mtaona. Ombeni, nanyi mtapewa.” Hilo ni rahisi tu jinsi hiyo.

¹³⁹ Sasa, ninajua jambo moja, ya kwamba popote ambapo kweli unampata Mungu, inakufanya ufanye mambo yasiyo ya kawaida. Unamwona Musa, kesho yake, baadaye. Alikuwa ametoroka kutoka . . .

¹⁴⁰ Alikuwa tayari ametoroka kutoka Misri, na alikuwa huko nje, na kumwoa Zipora, na alikuwa na mwanawe mdogo, Gershomu. Naye huyu hapa, tayari amesahau utumwa wa watu. Lakini Mungu alipomtokea pale katika kijiti kilichowaka moto; siku ya pili yake, alimpandisha Zipora juu ya nyumbu, na mtoto mdogo pajani mwake. Na ndevu zenye mvi zikining’inia mpaka kiunoni mwake; kichwa chake chenye upara kiking’ara. Na fimbo mkononi mwake akishuka, kupitia kule, “Utukufu kwa Mungu,” macho yake yakiangalia upande wa pili.

“Unaenda wapi, Musa?”

¹⁴¹ “Tunashuka kwenda Misri, kuiteka,” uvamizi wa mtu mmoja.

¹⁴² Loo, litakufanya ufanye mambo ya kuchekesha, lakini hilo ni sawa. Alimuradi unajua unakoelekea, hilo ni sawa.

“Unajua je kwamba utaiteka?”

“Mungu alisema hivyo.” Hilo linatosha. Hicho kilisema hivyo. “Mungu alisema hivyo.”

¹⁴³ “Loo, wewe una umri wa miaka themanini! Kama ungalifanya jambo hilo, ungalienda ulipokuwa na umri wa miaka arobaini.”

¹⁴⁴ “Lakini Mungu alisema, ‘Nenda sasa hivi. Wakati ndio huu.’” Uvamizi wa mtu mmoja, akishuka kwenda kuivamia.

¹⁴⁵ Mungu anakufanya utende mambo yasiyo ya kawaida, hata kama unaonekana kama propela ya kuonyesha uelekeo wa upepo iliyo juu ya jengo. Bali alimuradi ni Mungu anayefanya jambo hilo, mbona, ni sawa. Inaleta tofauti gani? Huenda ikaondoa baadhi ya mafundisho fulani ya theolojia ya Kibaptisti ndani yako. Bali ilimradi tu Mungu anafanya jambo hilo, Yeye hujifunua katika urahisi. Mhubiri huyo alijua mengi zaidi kuhusu Mungu, akitokea juu ya nyumba hiyo, kuliko mafunzo aliyopata miaka yote aliyoenda shuleni. Amina. Mungu hujifunua katika urahisi, kisha anajionyesha katika nguvu. Amina. Anajificha, kisha anajidhihirisha Mwenyewe. Anataka

kuona jinsi unavyokuwa rahisi, si jinsi unavyoweza kuwa mwerevu, bali jinsi unavyoweza kuwa rahisi.

¹⁴⁶ Mungu hujitambulisha katika urahisi, si katika werevu na ujanja. Hiyo ni ya Ibilisi. Hebu fuatilieni yale mafunzo. Ni wapi watoto wa Kaini, watoto wake walishikwa na nini? Watoto wa Ibilisi, nini kilichowapata? Wote walikuwa waalimu werevu, wanasayansi, na kadhalika. Hebu wafuatilie watoto wa Sethi: wanyenyekevu, wakulima wadogo, wafugaji wa kondoo, na kadhalika. Mwishoni mwa ulimwengu ule, nini kilichotukia? Mwishoni mwa ulimwengu uliotangulia ile gharika, ni nini kilichotukia? Wote walipotea. Walikuwa watu wa dini, pia. Bila shaka, walikuwa watu wa dini. Lakini, unaona, Mungu alimtuma Nuhu, akachukua watu walio wanyenyekevu, watu wa kawaida, na kuwapandisha juu. Ndipo watoto wa Kaini wakaangamizwa.

¹⁴⁷ Ni jambo lile lile leo, hao watu werevu, wajanja. Unaona? Hivyo ndivyo Shetani alivyomdanganya Hawa katika bustani ya Edeni. Hivyo ndivyo watoto wake walivyofanya huko nyuma kote.

¹⁴⁸ Angalia Moabu, lile shirika kuu na zuri likisimama pale juu ya kile kilima. Jamani, ni mahali pazuri jinsi gani! Sasa, hakuna. . . Wao wanaabudu Mungu yule yule. Maana, walienda na kumchukua askofu wao, Balaamu. Alitoka akaja pale na kuweka madhabahu saba, dhabihu saba. Madhabahu ile ile, dhabihu ile ile, kila kitu vile vile kabisa kama Israeli walivyofanya, maskini wale wazururaji chini kule. Na ndipo wakajaribu kumlaani ndugu yao, unaona, kumzuia asipitie katika nchi hiyo. Hawakutaka mmoja wa hao watu wa uamsho wa watakatifu wanaojifingirisha pale miongoni mwa watu wao. Ni nini kilichotukia? Mungu aliendelea moja kwa moja, hata hivyo, kwa maana waliahidiwa kwenda kwenye nchi ya ahadi, wala hakuna kitu kingaliweza kuwazuia. Mungu aliwashughulikia. Mungu akijificha katika urahisi, hivyo ndivyo anavyofanya daima, nao kwa kawaida hilo huwapita.

¹⁴⁹ Musa alikuwa mtumishi wa Kristo aliyewekwa wakfu. Ndipo Mungu. . . kwenye kile kijiti kilichowaka moto, alijua mengi zaidi juu ya. . . Musa alijua mengi zaidi juu ya Mungu wakati alipoondoka kwenye hicho kijiti kilichowaka moto kuliko miaka yote arobaini aliyojifunza juu Yake kule Misri. Tunajua hilo ni kweli.

¹⁵⁰ Katika siku za Ahabu, ulimwengu ulikuwa umefikia mahali fulani hivi kwamba, siasa zilikuwa zimehusishwa sana, kama tulivyozungumza juu ya jambo hilo asubuhi ya leo, mpaka Ahabu alipojitokeza jukwaani. Sasa, Ahabu hakuwa mtu mbaya. Yeye alikuwa tu Mwisraeli vuguvugu, aliyerudi nyuma ambaye aliacha mkewe amwongoze kila mahali. Mkewe alikuwa ni shingo iliyokigeuza kichwa.

¹⁵¹ Na hilo ndilo jambo lile lile tulilo nalo hapa Marekani sasa. Bila shaka. Sisemi, raisi wetu, *fulani*. Huenda akawa mtu mzuri. Lakini ni ule mfumo wa kale ndio unaoiongoza, huo ndio unaendesha mambo.

¹⁵² Ninyi liangalieni. Ninyi lizingatieni tu. Mnafikiri ninasimama hapa bure tu nikisema jambo ambalo sijui ninachozungumzia. Kumbukeni yale niliyowaambia. Naam, bwana. Mimi ninakuwa mzee. Sina siku nyingi zaidi zilizosalia hapa duniani. Kama Yesu akikawia kwa muda mrefu, nitaondoka hivi karibuni sana. Lakini huu utarekodiwa, nanyi mtausikiliza tena, na mtaona ya kwamba ilikuwa ni kweli. Mnaishi katika vivuli. Hakuna matumaini yaliyosalia, hata kidogo. Sasa, kumbukeni, mimi nikijua hilo, nikiwa mzee kama nilivyo, na nikisimama hapa nikijua ya kwamba wakati unaenda mbio sana. Na ninyi mme—mmekwisha. Taifa hili limekwisha. Kila kitu kimekwisha. Hiyo ni kweli. Na jambo pekee, “Jiepusheni na kizazi hiki kinachopelekeshwa,” maana kimekwisha. Hiyo ni kweli.

¹⁵³ Ahabu. Siku ile ambayo Yezebeli aliingia, akawafanya wanawake wote kutenda kama yeye alivyokuwa akitenda, na—nafikiri mambo aliyopitia, na Ahabu akaachilia hayo mambo. Na wahubiri wote wakawa wa kidunia.

¹⁵⁴ Lakini katika wakati uo huo, Mungu alimwinua mtu mwenye nguvu. Hata hatujui alitokea wapi. Hatujui baba yake na mama yake alikuwa ni nani. Haijulikani alikotoka, bali alienda Utukufuni. Hatujui baba yake na mama yake alikuwa ni nani, hakuna siku alipata kwenda shuleni. Alikuwa mtu wa nyikani. Hatujui alivyokuja. Alijitokeza tu jukwaani kwa jinsi isiyo ya kawaida, akaondoka jukwaani kwa njia isiyo ya kawaida. Basi akaja kule, ndipo Yeye akakitikisa kizazi hicho, akitumia mtu wa kawaida.

¹⁵⁵ Unafikiri wanateolojia waliwaziaje juu yake katika siku hiyo? Mbona, unafikiri walimkubali Eliya? Walisema, “Yeye ni mzee mwenye wazimu.” Yezebeli akasema, “Ninamchukia.” Na—na kila mtu alimchukia. Bali alikuwa na Neno la Bwana kwa ajili ya wokovu wa taifa hilo. Bali wasingeamini jambo hilo.

¹⁵⁶ Mtu wa aina ya kawaida tu, ndivyo Eliya alivyokuwa. Naye alitimiza kusudi la Mungu vizuri sana, hiyo roho nyofu ilikuwa ndani ya Eliya, hata Mungu akaitumia katika watu watatu wengine, tayari, na akaahidi kuitumia tena katika siku za mwisho. Naam, nyofu sana, ambaye anasimama tu na kusema Kweli. Aliitumia katika Elisha, baada yake. Akaitumia katika Yohana Mbatizaji. Akaiahidi tena, katika Malaki 4, “Kuirejesha imani ya watoto irudi kwenye Imani ya baba wa kipentekoste na Injili ya awali.” Ye—Yeye aliahidi jambo hilo, naye atalitimiza. Hiyo ni kweli. Hiyo roho nyofu, si yenye elimu, si erevu.

157 Eliya hakuwa msomi. Hakuwa mtu mashuhuri duniani. Yeye, hatujui alikotoka. Bali alikuwa na akili ya kutosha kumwamini Mungu. Mtu rahisi, hao basi, hao ndio namna ya watu ambao Mungu hufanya kazi nao, anaojificha ndani yao. Mungu alijificha katika Eliya.

158 Ungeweza kuwazia mtu kama Musa, mtu wa kawaida akifanya mambo aliyofanya?

159 Je! ungeweza kuwazia jambo hilo, Eliya, mzee aliyejaa mvi, amejaa nyele mwili mzima, amevaa kipande cha ngozi ya kondoo? Ungeweza kuwazia Mungu akichukua kitu kama hicho, wakati hapo walisimama makuhani na—na makasisi waliokuwa wamevaa majoho, nao wameng'arishwa katika teolojia yao, wapole sana walivyoweza kuwa? Lakini Mungu alimpita kila mmoja wao.

160 Yeye anafanya hivyo sikuzote. Niambie wakati mmoja aliopata kufanya hivyo. Hakuna. La, bwana. Yeye alivuka kitu hicho chote, apate kuja kwa mtu rahisi. Yeye hujifunua na kutenda kazi katika urahisi, kirahisi sana hivi kwamba kila mtu atalifahamu Hilo. Hilo ndilo linalomfanya kuwa mkuu. Yeye alikuwa rahisi, akirahisisha Hilo.

161 Na, sasa, Yeye alivuka. Ingawa ulimwengu ulikuwa umejaa wasomi mashuhuri katika siku ile, bali Yeye hakumtumia hata mmoja wao. Alijitafutia mtu rahisi. Lakini kumbukeni, aina hii ilikuwa katika wakati ule. Lakini, unaona, roho aliyokuja nayo ilikuwa ni rahisi kupita kiasi kulingana na elimu yao. Wao tayari walikuwa wamechora picha ya Hilo mawazoni mwao, kitu gani kingeweza kuja. Walikuwa werevu mno hata wakapitwa na urahisi Wake, na mara nyingine wanalivuka, wanalidhihaki.

162 Inanikumbusha juu ya methali ya kale, “Wajinga watatembea na viatu vya njumu mahali ambapo Malaika wanaogopa kukanyaga.”

163 Mtu ambaye ataona kazi za Mungu zikiendelea, na ajue ya kwamba ni kazi za Mungu kisha asimame na kuziita ni kazi za Ibilisi, Yesu alisema huko ni kukufuru. “Kama ukisema neno dhidi Yangu, Mwana wa Adamu, utasamehewa. Bali yeyote anayesema neno dhidi ya Roho Mtakatifu hatasamehewa hayo katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ule ujao.” Unaona? Bali tunatembea kwa viatu vya njumu mahali ambapo Malaika wanaogopa kupakanyaga.

164 Sisi, ni werevu sana. Tuna akili nyingi sana. Hivyo, hivyo ndivyo Marekani yetu inavyokuwa. Tuko na akili nyingi mno. Tunajielimisha wenyewe mbali na Mungu. Shule zetu zinawatuma wahubiri wetu kama kuku wa mtambo wa kuatamia.

165 Daima nimemsikitikia kuku wa mtambo wa kuatamia. Yeye alianguliwa chini ya nuru ya bandia. Na muda si muda unajua,

yeye angemlilia mama “chwi, chwi”, kwa maana hiyo ndiyo asili yake. Bali hana mama. Yeye alianguliwa kwa kiangulio.

¹⁶⁶ Hivyo ndivyo ninavyofikiria kabisa kuhusu digrii hizi zinavyofanya, kuku wa kiangulio, mkililia kitu ambacho hamjui mnachozungumzia. Hiyo ni kweli. Wakati, mna mfano wa utauwa, na mnakana Neno hilo, na mnakana ya kwamba Roho Mtakatifu si yeye yule leo kama alivyokuwa siku aliyomwaga Pentekoste.

“Walisema huyo alikuwa ni kwa ajili ya wale wanafunzi.”

¹⁶⁷ Yesu alisema, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Kwa muda gani? “Hata ukamilifu wa dahari, na kwa kila kiumbe, ishara hizi zitafuatana nao.” Bila shaka. Waambie... Nitakuonyesha mahali ambapo Yeye alilipa Kanisa nguvu. Wewe nionyeshe mahali ambapo aliziondoa. Hakuna. La.

¹⁶⁸ Lakini, unaona, tunakuwa werevu sana, tunajielimisha mbali nalo. Tunapata misamiati na mambo chungu nzima tunayoshughulikia. “Vema, hayo yanahoji, hilo ni jambo lile lile tu. Vema, sasa angalia, tuna madaktari wazuri,” tunasema, “leo. Kwa nini tutake uponyaji wa Kiungu?”

¹⁶⁹ Angalia yale ambayo yule daktari mzuri aliyosema muda kidogo uliopita. Anafikia kikomo cha wajibu wake, ndipo anamtumaini Mungu. Haya basi. Jambo ndilo hilo. Sayansi ni sawa, ilimradi tu unaupanda mti. Na wakati unapofikia juu sana, huwezi kwenda juu zaidi, nenda kwenye mti wa imani na uendelee tu kutembea, unaona, kwa sababu ha—hauna mwisho. “Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.” Naam. Naam.

¹⁷⁰ Sayansi ni sawa, umbali inaoenda. Hisi zako tano ni nzuri na ni sawa kabisa, mradi tu zinakubaliana na Neno. Bali wakati hizo hisi tano zinapolihukumu Neno, basi achana nazo. La. Nisingeamini kuhisi kwangu, nisingeamini kusikia kwangu, nisingeamini kuona kwangu, chochote kile, kama ni kinyume cha Neno. Nitasema ni- . . .

¹⁷¹ Jamaa fulani aliniambia, wakati fulani uliopita, kasema, “Sijali ni watu wangapi ninyi Wapentekoste mngeweza kuthibitisha ya kwamba waliponywa. Mimi siamini hilo.”

¹⁷² Nikasema. “Bila shaka huamini. Wewe ni asiyeamini. Haikuwa kwa ajili ya wasioamini. Ni kwa ajili ya waaminio.” Barabara. Hakika. Haikuwa... Halikutumwa kwa wasioamini. Lilitumwa kwa hao wanaoamini.

¹⁷³ Yesu alikuja, moja kwa moja katika siku ya kutokuamini. Hakukumzuia. Yeye aliendelea tu kuhubiri moja kwa moja, vivyo hivyo tu. Mungu alifanya miujiza, vivyo hivyo tu, katika uliwengu huo maarufu wenye elimu.

¹⁷⁴ Tunaishi katika ulimwengu maarufu wa kielimu leo, kupasua atomu, na kutengeneza mabomu, na kadhalika, na

kuruka kwenda mwezini, na wanaanga, na chochote kile kote ulimwenguni. Hilo ni kweli. Tunafanya hayo. Hayo ni sawa.

¹⁷⁵ Lakini, hata hivyo, kuna watu wanaoamini ya kwamba huo ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kama tu ulivyokuwa sikuzote. Hawawezi kuuelezea, bali wanajua waliupata. Hivyo ndivyo tu ilivyo. Haikulazimu kuuelezea, ilimradi tu unao. Amina.

¹⁷⁶ *Amina* maana yake ni “na iwe hivyo.” Mimi sijiitikii amina mwenyewe. Lakini ni—ninaninii tu... Ninapenda Neno. Kwa hiyo na iwe hivyo! Na—najua hiyo ni kweli.

¹⁷⁷ Mungu anajifanya wa kawaida sana hivi kwamba anapita kabisa juu ya... Wenye hekima ni werevu sana, ile akili ndogo ya njugu, unajua. Wamekwisha wazia vile yote yatakavyokuwa. Huwezi kuwaambia kitu kuhusu jambo hilo. Dunia haiwezi kusogea, jua haliwezi kuwaka, dunia haiwezi kuzunguka, bila ya wao kujua, unaona. Bali Mungu anaruka moja kwa moja juu ya vichwa vyao na kuwaacha tu waketi pale. Hivyo ndivyo tu Yeye amefanya daima. Naam, bwana.

¹⁷⁸ Huko nyuma kote tangu bustani ya Edeni, Masihi alitabiriwa kwamba atakuja. “Uzao wako utakiponda kichwa cha nyoka, na kichwa chake kitaponda kisigino.” Loo, jamani! Lilisema. Manabii walitangulia kumwona, na wakatabiri juu ya alama vile ambavyo Yeye angekuwa, wapi angezaliwa, angezaliwaje, kwamba angefanya kazi ya namna gani, kwamba ishara Yake ya Kimasihi ingekuwa ni nini. Maandiko yaliypangilia vizuri yote kote kote.

¹⁷⁹ Lakini wanathiolojia walikuwa wameyawazia yote, namna yao, nao wakamkosa kwa maili mia moja. Lakini Yeye kamwe hakuja kinyume na Neno. Alikuwa kulingana na Neno. Lakini kwa nini wao hawakumpokea? Ni kwa sababu Yeye hakuja vile walivyofikiri anapaswa kuja. Hivyo ndivyo hasa walivyokosa kumwona Nuhu. Hivyo ndivyo walivyokosa kumwona Musa. Hivyo ndivyo walivyolikosa, katika nyakati zote huko nyuma.

¹⁸⁰ Wanashindwa kuona urahisi wa Mungu akitenda jambo fulani. Unaona? Mungu hujificha Mwenyewe pale. Naye anapita tu juu ya ninii—ya wenye hekima na akili, kwa maana Yeye ni mkubwa sana. Unaona? Hebu chukua vitu viwili vikija kukutana pamoja, namna *hii*, na wakati vinapopitana, unaona ninaloamaanisha? Hivyo ndivyo Mungu anavyoweza kufanya. Yeye anaweza kuwa rahisi sana mpaka anaweza kwenda mbali sana na mtu fulani mpaka hawawezi kuona mahali alipo. Amina. Ninapenda hilo. Nina furaha Yeye amelifanya namna hiyo, ndipo basi ninaweza—ninaweza kulikubali. Kwa kuwa, kuna elimu fulani nisingejua nifanye nini nayo. Lakini Yeye alilirahisisha sana, watu kama mimi wangeweza kulifahamu, ama kuliamini. Kwa hiyo, ninashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo.

¹⁸¹ Sasa, Masihi alitabiriwa, jinsi angekuja, mahali angezaliwa, kile angefanya, kile huduma Yake ingekuwa, na kwamba

angefika wakati gani. Lakini, wakati alipowasili, hao wahudumu na makasisi wa siku hiyo walikuwa na mapokeo mengi sana, nao walikwisha fikiria vile hasa jinsi ambavyo Yeye angekuja. Na Mfarisayo anasema, “Kama akija, atakuwa Mfarisayo.” Msadukayo anasema, “Upuuzi: si na kundi hilo la wanaojisingizia kwamba ni wenye haki. Yeye atakuwa Msadukayo.” Lakini alipokuja, wala hakuwa mmoja wao. Kamwe hakuulizia ninii zao... haikumlazimu Mungu kuulizia ninii zao... sehemu ya hekima yao, jinsi ya kumtuma Mwanawe.

¹⁸² Yeye alilituma jinsi alivyosema angelituma. Yeye alikuja kulingana... Na akaleta... Na mtu ulipozungumza juu ya Masihi wao kutangazwa kwenye hori, juu ya lundo la mbolea, kwenye zizi la ng’ombe; je! kundi la Mafarisayo werevu, wanaojisingizia ni wenye haki, wanafiki wenye mbwembwe wangetarajia kitu kama cha Masihi wao ajitokeze kwenye zizi la ng’ombe? Vema, ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni Yehova, maskini Yehova akilia kama mtoto mchanga. Je! wangeweza kumtarajia yule Yehova wa kutisha, aliyenguruma kutoka Mlima Sinai, aliyeuwasha moto mlima huo, aliyeifungua Bahari ya Shamu, kufanyika Mtoto Mchanga kwenye zizi? Loo, hilo, thiolojia yao isingeweza kumeza hilo. La, hata kidogo, si Masihi wao.

¹⁸³ Wao walisema, “Mungu atakapomtuma Masihi, hapana shaka, atashusha chini kumbi za Mbinguni. Atashusha gwaride la Malaika elfu kumi. Atakuja moja kwa moja kwenye hekalu ambalo Musa alituachia, ama tulilojengewa na Sulemani hapa. Naye atakuja moja kwa moja kwenye hekalu hili, naye atatukubali papa hapa. Na kuhani wetu mkuu ambaye tumemchagua, kiongozi wetu, mwakilishi wetu wa jimbo, ama chochote kile, Yeye atakuja kwake na kusema, ‘Nimewasili. Mimi hapa. Mimi huyu. Mimi ndiye Masihi. Hivi hamnitambui? Unaona, ushoroba utashuka. Ninatoka Mbinguni.’” Hivyo ndivyo walivyokuwa wameyawazia.

¹⁸⁴ Lakini wakati alipokuja, alikuwa kwenye banda la ng’ombe, akazaliwa na mama ambaye... na baba ambaye alikuwa na—na historia haramu juu yake, ilivyoonekana, kama walivyodhani. Amefungwa katika nguo Zake za kitoto, wananiambia, zilikuwa zimetolewa kwenye nira ya maksai, alikuwa maskini jinsi hiyo. Mungu aliyeumba mbingu na nchi na kufanya kila kitu kwa Yesu Kristo; na hapa alikuwa yupo Muumba Mwenyewe, Mungu, Aliyeumba mbingu na nchi, akilala kwenye hori, katika lundo la nyasi kavu ambazo Yeye, Mwenyewe, alikuwa ameziumba. Muumba wa mbingu na nchi alijinyenyekeza, apate kuwa wa chini kuliko wote. Aliye Juu zaidi akiwa aliye chini zaidi, hilo ndilo lililomfanya Mungu. Hilo ndilo lililomfanya kile alichokuwa. Unaona, alijinyenyekeza. Mwanadamu asingeweza kufanya jambo hilo.

¹⁸⁵ Unamwinua mtu, hebu mpe tu mamlaka ki—kidogo tu katika madhehebu, ndugu, huwezi kupita karibu naye. Ndiyo

mambo yalivyo. Ndiye mwenyewe hasa! Amefura kama chura anayelipuliwa risasi. Usinge—usingeweza kufanya chochote naye. Lakini, lakini, unaona.

¹⁸⁶ Lakini, Mungu anaweza kujidhili kwa sababu Yeye ni mkuu sana. Yeye amezidi kile tunachoita kikuu. Yuko upande ule mwingine. Naye ni mkuu sana hata anaweza kujishusha Mwenyewe. “Ninakushukuru, Baba, wa mbingu na nchi ya kwamba ume-yaficha mambo haya wenye hekima na akili.” Kama nilivyosema, tunapasua atomu wala hatuwezi kuelezea uhai katika jani la unyasi. Unaona? Tunatembea juu yake, kitu kile hasa ambacho humtangaza Mungu. Tunaruka.

¹⁸⁷ Hilo ndilo jambo lile lile tunalofanya leo. Ndiyo, bwana. Tunavuka juu ya *Hili*, ambalo ni Mungu katika andiko, hiyo ni kweli, na kukubali kanuni fulani ya imani ya mwanadamu ama fundisho la sharti badala Yake. Kuuza haki yenu ya mzaliwa wa kwanza kwa bakuli la uji, kwa ajili ya sifa, kwa ajili ya kanisa litakalokuruhusu kukata nywele zako na kuvaa kaptura, na kukupeleka kwenye tafrija za pombe kali na vitu kama hivyo, na halafu unajiita wewe ni Mkristo. Aibu kwako. Kweli.

¹⁸⁸ Si eti ninawakaripia; bali—bali kwa heshima za kiungu na upendo. Hiyo ni kweli. Tokeni kwenye jambo kama hilo. Rudini kwa Mungu na Biblia Yake. Rudini kwenye Kweli ya Injili. Naam. Ati unaachilia madhehebu fulani yakufunge kukuondoa kwenye mambo ya Mungu? Kamwe usifanye jambo hilo. Rudi kwenye njia rahisi ya Mungu. Anguka tu magotini mwako na useme, “Bwana Mungu, sijali nini, jinsi gani utakavyonipa Huo, bali niko hapa kwa ajili Yake.” Angalia jambo litakalotukia. Uwe mnyofu juu ya jambo hilo.

¹⁸⁹ Ana shauku zaidi ya kukupa wewe Huyo kuliko ulivyo na hamu ya kumpokea. Haikulazimu kungoja, na kungoja, na kungoja. Hakuna kitu kama hicho. “Petro alipokuwa akisema Maneno haya, Roho Mtakatifu aliwashukia wale waliolisikia.” Naam. Shida yake ni kwamba, hatumwonei shauku vya kutosha. La, hasha. Hatutaki kujinyenyekeza. Hiyo ni kweli.

¹⁹⁰ Nilikuwa nikihubiri hapa, si muda mrefu uliopita, na kulikuwa na bibi fulani aliyefurahi sana, naye akaanza kupiga makelele. Kulikuwa na mvulana mmoja ambaye hucheza besiboli mjini. Akasema, “Billy, nilikuwa nimesimama huko nje. Nisingeweza kuingia.” Akasema, “Nilikuwa nikifurahia ujumbe wako mpaka mwanamke hu—huyo alipoanza kulia na kuendelea namna hiyo.” Akasema, “Ndipo watu hao wote basi wakaanza kupaza sauti na kupiga makelele.” Akasema, “Hilo liliniletea kusikia baridi ikishuka mgongoni mwangu.”

“Loo,” nikasema, “hivi hukuamini jambo hilo?”

Akasema, “Hapana.”

¹⁹¹ Nikasema, “Kama hawakufanya hivyo, lingenifanya nisikie baridi ikishuka mgongoni mwangu.” Uaona? Nikasema,

“Nisingejua mahali nilipokuwa nikipazungumzia, kile nilichokuwa nikisema habari zake.” Unaona?

¹⁹² Na kwa hiyo akasema . . . Alikuwa shabiki wa besiboli. Nami nikabadilisha . . . Akasema, “Vema, ni nani aliyepata kusikia kitu kama hicho?” Alikuwa mfuasi wa kanisa lile lile la kimadhehebu nilimotoka mimi. Ndipo akasema, “Vema, sasa, Ujumbe wako ulikuwa sawa, kile ulichokuwa ukinena habari zake. Lakini ni nani angeweza kukusikia?”

¹⁹³ Nikasema, “Wakati huo haikuwa ni kuhusu ‘kusikia.’ Roho Mtakatifu alikuwapo. Alikuwa tayari ameshika hatamu.” Unaona? Nikasema, “Anapokuja ni wakati wa mimi kunyamaza, unaona, Naye ameingia miongoni mwa watu.”

¹⁹⁴ Akasema, “Ha-ha-ha, Billy,” kasema, “wewe ni mshupavu tu wa dini. Ndivyo ilivyo.”

¹⁹⁵ Nikasema, “Vema, labda ndivyo nilivyo.” Nikasema, “Kama ndivyo nilivyo, mimi ni mmoja wa washupavu wa dini walio na furaha sana uliopata kuona.” Unaona? Ndipo nikasema, “Mimi . . .”

Akasema, “Vema, ninataka kukwambia.” Nikaanza kuzungumza naye.

¹⁹⁶ Nikasema, “Aisee!” Na uwanja wa besiboli hauko mbali na nyumba. Nikasema, “Ni kitu gani basi kilichokuwa kikitukia kule, hivi majuzi usiku?”

¹⁹⁷ Akasema, “Laiti ungalionga jambo hilo!” Kasema, “Unamjua Charles Nolan? Aisee! Watu watatu kituoni!” Naye akahemukwa kabisa.

¹⁹⁸ Nikasema, “Vema, enyi kundi la wasio wafingirikaji wachafu, sijapata kusikia kelele kama hizo maishani mwangu.” Nikasema, “Kama ningalikuwa huko, nisingesema mengi sana juu yake. Ningalisimama tu na kuangalia.”

Akasema, “Wewe, basi, hujishughulishi sana na besiboli.”

¹⁹⁹ Nikasema, “La, hashu.” Nikasema, “Sijali mambo ya besiboli, kwa hiyo hainivutii.” Nikasema, “Kama ningekuwa ninavutiwa nayo, ningekuwa nikifanya kama wewe. Na kama wewe ungelikuwa unavutiwa na Mungu wangu, na kule Kuja kwa Bwana Yesu, na nguvu za Mungu, ungelikuwa ukifanya jinsi hiyo hiyo wakati Roho Mtakatifu anaposhuka ndani ya jengo.”

²⁰⁰ Inategemea ni roho wa aina gani aliye ndani yako, kile unachokula. Uhai wako unakula kitu fulani. Ndipo nikasema, “Usiwe nderi anayekula mizoga ya nyama zilizooza za siku nyingi za ardhini. Kula vitu vya Mbinguni, Neno la Mungu. Yesu alisema, ‘Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.’” Kula Neno Lake. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

201 Kwa hiyo wakati Yesu alipokuja, walikuwa wameshawazia atakavyokuwa mpaka wakamfanya Yeye kuwa ni mkuu sana. Hawakuweza kuona jinsi Mtu mkuu namna hii angaliweza kuzaliwa kwenye hori la ng'ombe. Hawangeweza kuona jinsi ambavyo mtu mkuu namna hiyo angeweza kuwa rahisi hivyo.

202 Ni jambo lile lile siku hizi. Watu wanafikiri ya kwamba dini, dini ya Kikristo, inapaswa kuwa na kanisa kubwa mno, jengo kubwa mno, kinanda kikubwa mno cha zumari cha dola milioni moja, benchi nzuri sana za anasa.

203 Uliwahi kufika Ireland? Ulipata kuona Mtakatifu Patrick, ambaye ninyi Wakatoliki mlimwita Makatoliki? Alikuwa tu kadiri nilivyo Mimi. Kwa hiyo ulipata kwenda huko juu? Wala hata asingeweka msalaba wenye sanamu uning'inie nyumbani mwake. Alipinga kanisa la Rumi kwa nguvu sana alivyoweza. Hata asingewaruhusu watu kuketi. Aliwaacha wachuchumae juu ya kipandio cha ubao wa—wa kale, si ubao, bali mwamba hu—humo jengoni. Jengo lake lingali linasimama kule. Aliwafundisha ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mtakatifu Francis, na mtakatifu. . .

204 Na hao watengenezaji mashuhuri wa siku za mwanzoni na watu wa zamani huko nyuma katika siku hizo, jinsi walivyofundisha ubatizo wa Roho Mtakatifu! Jinsi ambavyo Mtakatifu Martin, Ireneo, wale watu mashuhuri, walivyofundisha ubatizo wa Roho Mtakatifu! Wasingewaacha watu hao wastarehe, na waketi hapo kwenye viti vya anasa na mambo kama tunayofanya siku hizi. Na hata hivyo tunaliita hilo kuwa ni kanisa lililofanikiwa. Mwanadamu anaita ufanisi, wakati mwingine, dini.

205 Ilisemwa huko California ya kwamba “Mtu si wa kiroho mpaka aweze kuwa na kadilaki tatu.” Kwa maoni yangu, hapo ndipo anapomwacha Mungu. Hiyo ni kweli. Kanisa la Kipentekoste leo hakika linatenda ilivyo tofauti na vile Kanisa la kipentekoste la mwanzoni lilivyofanya.

206 Nilikuwa nikizungumza kwenye mkutano wa Wafanyabiashara Wakristo wakati mmoja, sehemu fulani. Sijui jinsi walivyopata kunialika tena. Nadhani, ni kwa sababu wananipenda. Lakini mi—mi—mimi sininii. . .

207 Ninawaambia yale tu mimi ni—ninayojua Bwana anasema. Sisemi hayo kujionyesha kuwa nina akili. Kama nikifanya hivyo, ninahitaji kuwa kule chini madhabahuni. Ninasema jambo hilo kwa sababu ninawapenda. Ninawaheshimu.

208 Usiku mmoja kule chini, wakiwa wanashuhudia mbele za wafanyabiashara wa dunia, kwamba wana kadilaki ngapi, na juu ya biashara zao ndogo. Nilisema, “Hao watu hawataki jambo hilo. Waambie juu ya unyenyekevu wa Kristo.” Nikasema, “Ninyi mko tofauti sana na Kanisa la la mwanzoni la Kipentekoste. Wao waliuza kila kitu walichokuwa nacho, na kuwapa maskini, kisha

wakatoka wakaenda kuihubiri Injili.” Nikasema, “Ninyi watu mnajaribu kusema kadiri mlivyofanikiwa, kwamba mna mali nyingi kiasi gani.” Si suala la kiasi gani ulicho nacho; ni suala la kiasi gani unachoweza kutoa!

²⁰⁹ Nikawazia, jamaa yule jana usiku, akinena juu ya jambo lile lile. Maskini ndugu fulani mmoja mpentekoste kutoka Chicago alisimama. Akasema, “Ndugu Branham, ningetaka kukupa changamoto.”

Nikasema, “Nipe.”

Basi akasema, “Hapo ndipo Kanisa lilipofanya kosa.”

Nikasema, “Ati Roho Mtakatifu afanye kosa? Hawezi.”

²¹⁰ Akasema, “Alikosea hapo. Unaona, wakati mateso yalipozuka, hawakuwa na makazi yoyote ya kwenda.”

²¹¹ Nikasema, “Mapenzi ya Mungu kabisa. Ndipo wakaenda kila mahali, wakieneza Injili, maana hawakuwa na mahali pengine pa kwenda.” Huwezi kumshinda Mungu. Naam, bwana. Mungu aliuza tu kila kitu kilichokuwa mikononi mwao, ili kwamba wasipate mahali popote pa kwenda, ndipo tu wakaenda wakihubiri kila mahali, njia pekee ambayo Mungu angeweza kuwafanya waende.

²¹² Lakini, siku hizi, tunapenda kuzimisha, mnajua, na kuketi kwa starehe. Na kama mchungaji akisema kitu chochote tusichopenda, katika Assemblies, basi tunahamia kwa Umoja. Akisema chochote ambacho hatutaki, vema, hatimaye, tutaishia katika Baptisti ama Presbiteri, ama mahali fulani ambako tunaweza kufanya lolote tunalotaka kufanya. Jambo—jambo ndilo hilo. Hao ni sisi. Halafu ati tunajiita “Wakristo”? Unataka ninii . . .

²¹³ Mnapigia kura mchungaji wenu, wengi wenu, kanisani mwenu. Na mnapofanya hivyo, mnataka msomi aliye na elimu ya juu kabisa, ili muweze kuwaambia majirani zenu, “Mchungaji wetu ana digrii ya da—daktari, Dkt. wetu *nanii*.” Loo, jamani! Mnaninii—mnajiondoa kwa Mungu. Mnaninii . . .

²¹⁴ Mungu hujifunua katika urahisi. Sikilizeni. Hilo lilikuwa limezidi mno kwa wale watu wa hali ya juu, wataalamu, wasomi wa siku hizo. Mungu akijificha katika urahisi, katika Mtoto mchanga.

²¹⁵ Hebu angalia wakati walipomsulibisha, loo, hilo liliwapata juu ya alama. Miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, alasiri hii, walimsulibisha Mfalme wa Uzima. Wakati, hao makuhani wakuu waliokuwa wameshangaa, wakati wanamwona akifanya miujiza aliyofanya, na wakijua ya kwamba Yeye aliyahukumu madhehebu yao. Aliyavua nguo. Aliyachuna ngozi. Na akawaambia ya kwamba hawakuwa kitu ila kundi la pepo wachafu, na, “Tubuni!” Nao wakaninii . . .

216 “Mungu anaweza katika mawe haya,” Yohana alisema, “kumwinulia Ibrahimu watoto. Msifikiri ninyi ni watoto wa Mungu ati kwa sababu mmezaliwa Myahudi. Na kwa hiyo Mu- . . .” Alisema, aliwaita pale, “nyoka nyasini,” na kila kitu.

217 Ndipo wakati aliposimama pale msalabani, walisema, “Sasa, kama Wewe ni Mwana wa Mungu, kama Wewe ukiwa ndiye huyo Mwana wa Mungu, mbona usishuke kutoka msalabani nasi tutakuamini.” Unaona? Mambo yale yale. Wakati wangeweza kuwazia juu ya Mtu huyu akifanya muujiza, basi wasingeweza kukana jambo hilo. Bali kumwona Yeye amesimama pale, Mungu Mwenyewe wa uumbaji!

218 Sasa, ninajua mwelekeo huu wa siku hizi unajaribu kumfanya Yeye kuwa ni mtu mwingine. Bali Yeye hakuwa mtu mwingine ila Mungu Mwenyewe. Hiyo ni kweli. Leo, mwelekeo wa siku hizi ulisema, “Yeye alikuwa mwalimu mashuhuri. Alikuwa—alikuwa nabii.” Alikuwa mwalimu mashuhuri, na alikuwa nabii. Bali alikuwa zaidi ya mwalimu. Alikuwa zaidi ya nabii. Yeye alikuwa Mungu, hakuwa kitu pungufu ya Mungu.

219 “Mungu alikuwa katika Kristo, akiipatanisha nafsi Yake na ulimwengu.” Yesu alisema, “Si Mimi ninayefanya mambo haya. Ni Baba Yangu, Naye anakaa ndani Yangu. Ni Baba aliye ndani Yangu.” Alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili.

220 Mwanamke fulani wa madhehebu ya Sayansi ya Kikristo alinirii. . . Samahani, sikukusudia kutaja jina hilo sasa. Nina—ninasikitika nililitaja hilo. Bali yeye aliniambia, akasema, “Bw. Branham, ninafurahia mahubiri yako, lakini,” akasema, “unamsifu Yesu sana kupita kiasi.”

221 Nikasema, “Asante. Kama hayo ndiyo yote ninayofanya, ambayo ni ma—mabaya sana,” nikasema, “basi nina hakika ya kuingia Mbinguni.” Nikasema, “Laiti ningalikuwa na lugha milioni moja zaidi ambazo ningeweza kumsifu Yeye kwazo.”

222 Akasema, “Naam, mnampa Yeye sifa isiyokuwa Yake.”

Nikasema, “Yeye ni yote kwangu.”

223 Naye akasema, “Vema, sasa, ninaweza kukuthibitishia. . . Wewe unamfanya Mungu.”

224 Nikasema, “Yeye alikuwa Mungu. Kama hakuwa Mungu, Yeye ni mdanganyifu mkubwa sana ulimwengu uliyewahi kuwa naye.” Nikasema, “Yeye alikuwa Mungu. Yeye si chochote pungufu ya Mungu.”

225 Damu Yake Mwenyewe ilikuwa Mungu. Tunaokolewa kwa “Damu ya Mungu.” Yeye hakuwa Myahudi, wala hakuwa Mmataifa.

226 Jinsia ya mwanamume hutoa himoglobini. Daktari anajua hilo. Kuku anaweza kutaga yai, bali kama hakuwa na ndege dume, halitaanguliwa. Halikutunga. Hiyo ni kweli. Unaona? Linapaswa. . . Seli ya damu inatoka kwenye jinsia ya kiume.

227 Na katika jambo hili, Yehova Mungu alikuwa wa kiume. Yeye aliumba seli ya Damu ndani ya Mariamu.

228 Na ninyi Wakatoliki mnamwita “mama wa Mungu.” Angeweza kuwa mama wa Mungu, na Mungu hana mwisho na ni wa Milele? Yeye hakuwa mama ya Mungu. Alikuwa kiangulio ambacho Mungu alitumia, kumleta Mwanawe hapa. Bila shaka.

229 Lakini kasema, “Yeye alikuwa ndilo hilo yai? La, bwana. Kama angalikuwa hilo, ingembidi kupata msisimko, basi angalia kile unachomfanya Mungu.

230 Yeye aliumbwa kabisa, Mungu, Mungu wa uumbaji akiumbwa katika umbo la Mwanadamu. Hiyo ni kweli kabisa. Na alipoinii . . .

231 Akasema, “Mbona, ninaweza kukuthibitishia kwa Biblia yako mwenyewe ya kwamba Yeye hakuwa kitu chochote ila mwanadamu.”

Nikasema, “Endelea.”

232 Basi akasema, “Wakati Yeye, katika Yohana 11, Yeye aliposhuka kwenda kumfufua Lazaro.” Na akasema, “Alipoenda, Biblia ilisema, ‘Alilia.’” Na akasema, “Ilionyesha ilibidi awe mwanadamu, la sivyo asingeweza kulia.”

233 Nikasema, “Hoja hiyo ni nyepesi kuliko mchuzi uliopikwa kutoka kwenye kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa.” Nikasema, “Usijaribu kuniambia hilo.”

234 Nikasema, “Ninataka kukwambia jambo fulani. Wakati aliposhuka kwenda kule kaburini, ilikuwa ni kweli, Yeye alilia. Alikuwa Mwanadamu, wakati akilia. Bali wakati alipoukusanya mwili Wake mdogo, mwembamba, pamoja, akasema, ‘Lazaro, njoo huku!’ Na mtu, aliyekuwa amekufa kwa muda wa siku nne, akasimama kwa miguu yake na akaishi tena. Huyu alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, ambaye aliweza kufufua wafu. Huyu alikuwa ni Mungu ndani ya Mwanawe.” Kweli kabisa.

235 Ilikuwa kweli, aliposhuka kutoka mlimani usiku huo, akiwa na njaa, akitafuta kitu cha kula, aliangalia juu ya mti huo na asingeweza kupata chochote cha kula, ndipo akaaulaani ule mti. Huyu alikuwa ni Mungu, mwenye njaa. Bali alipochukua biskuti tano na vipande viwili vya samaki, na kuwalisha watu elfu tano, huyo alikuwa ni Muumba, Mungu ndani ya Mwanawe. Yeye alikuwa ninii . . .

236 Alikuwa Mwanadamu wakati amelala nyuma ya kile chombo usiku ule, wakati pepo elfu kumi wa baharini walipoapa ya kwamba watamzamisha. Maskini chombo hicho kidogo kikiyumba huku na huku, kama kizibo cha chupa nje kule. Alikuwa Mwanadamu amelala pale, amelala usingizi. Nguvu zilikuwa zimentoka. Bali wakati alipoweka mguu Wake kwenye demani, katika kile chombo, akaangalia juu na kusema, “Amani, tulia,” na upepo na mawimbi yakamtii Yeye, huyo alikuwa ni

zaidi ya Mwanadamu. Huyu alikuwa ni Mungu akizungumza kupitia Kwake. Yeye alikuwa Mungu-Mtu.

²³⁷ Wasingeweza kuona jambo hilo. Na hapo masalabani, walisema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, jiokoe Mwenyewe,” yule mwizi alimwambia. “Na kama Wewe Ndiye yule Masihi, shuka msalabani. Tuonyeshe. Kama Wewe Ndiye Mfalme wa Wayahudi, kama Wewe Ndiye, huyu, shuka na utuonyeshe.” Unaona, hiyo ingekuwa ni kuonyesha mamlaka.

²³⁸ Mungu alikuwa akijinyenyekeza katika urahisi, akichukua umbo la mauti. Mungu, Uhai wa namna ya juu kabisa, akawa wa uhai wa chini kabisa, akalaaniwa na maisha, mwenye dhambi, apate kufa, kusudi alete ufufuo. Loo, jamani! Mungu akijificha Mwenyewe katika mauti, apate kujionyesha katika ufufuo. Mungu, Uhai wa hali ya juu kabisa, Uzima wa Milele, akimfanya Mtu, mwili, kwa ajili Yake Mwenyewe apate kuishi ndani yake, akafanyika uhai wa hali ya chini kabisa, mwanadamu, aliyelaaniwa na Mungu. Na akachukua ile laana, juu ya nafsi Yake, na akafa, akijificha kutoka kwa hao wasomi wenye elimu.

²³⁹ Wakati Ibilisi alipomchukua akampeleka kule, nao wakamfunga tambara machoni Mwake, na kumpiga kichwani, na kusema, “Sasa, sisi, wananiambia Wewe ni nabii. Hebu tabiri sasa na utwambie ni nani aliyekupiga. Tutakuamini.” Ndipo wakapitishiana ile fimbo, wao kwa wao. Kamwe hakufungua kinywa Chake. Walipomtemea mate usoni, wakang’oa konzi chache za ndevu. Wakasema, “Loo, kama huyo...” Ibilisi akasema, “Kama huyo alikuwa ni Mungu, tulimpata. Kwisha.” Loo, mwangalie pale, haidhuru. Yeye alikuwa ni Mungu. Wakati alipokuwa akipaa juu...

²⁴⁰ Hebu na tuchukue kamera yetu na tuelekeze huko nyuma kwenye hiyo alasiri yenye giza, miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, alasiri ya leo. Mwangalie akipanda kile kilima. Ninasikia mshindo. Ni kitu gani? Ni msalaba wa kale unaoparuza ukipanda kwenda kwenye mimba ya kilima. Unakokota alama za nyayo zenye Damu ya Mbebaji, unapogongagonga kwenye hiyo miamba, ulipokuwa unashuka kwenda barabarani.

²⁴¹ Ninaangalia mgongoni Mwake mwote, ni vidoa vidogo vidogo kila mahali kwenye hilo joho lisilo na mshono. Mungu wa viumbe vyote akiubeba msalaba ambao kabisa Yeye aliuumba. Pale, Damu ya Imanueli imeanza kuonekana mgongoni, katika vidoa. Anapopanda kilima, vidoa hivyo vinazidi kuwa vikubwa zaidi na zaidi. Mara, vyote vinakuwa doa moja kubwa la Damu. Inaanza kutiririka kupitia kwenye miguu yake midogo, minyenyekevu, midhaifu. Ilikwa ni kitu gani? Akainamisha bega Lake, nguvu zake za kibinadamu. Hiyo ilikuwa ni nini? Mungu, Mungu akijificha katika urahisi. Huyu alikuwa ni Mungu akibeba huo msalaba.

242 Huyu hapa anapanda juu ya kilima, akijikwaa, hiyo hapo Damu inatiririka kutoka Kwake. Akaanguka. Simoni akauchukua msalaba, amsaidie kuubeba.

243 Akiwa anapanda kilimani, Ibilisi akasema, “Unajua nini?” Kasema, “Ninajua sasa ya kwamba Yeye si Mungu. Ninajua Yeye siye. Asingefanya hivyo kamwe. Nimempata sasa. Nimemshinda kila mwanadamu. Nimempata. Kwa hiyo ninajua huyo si Mungu.”

244 Kwa hiyo akamtuma nyuki wa mauti, amuume; na wakati huyo nyuki alipoanza kumzunguka akivuma, unajua, nyuki, wadudu walio na miiba. Na mauti yana mwiba. Lakini, unajua, kama mdudu akiwahi kuchoma sana, anachomoa mwiba wake. Kwa hiyo kama huo mwiba uliwahi kumdunga mtu, mtu wa kawaida . . . kama Yeye angalikuwa ni mtu tu wa kawaida, nabii. Yeye alikuwa amewadunga manabii wengi, na akafa. Bali wakati alipomuuma Huyu, alipoteza mwiba wake. Hakuwa na mwiba mwingine baadaye. Mungu; yeye alimdunga Imanueli mwiba wake, ndipo akachomoa mwiba huo kutoka kwenye mauti.

245 Miaka michache baadaye, wakati walipokuwa wakienda kumwua mmojawapo wa mitume Wake, yule Mtakatifu maarufu Paulo, alipaza sauti akasema “Ee mauti, uko wapi mwiba wako? Kaburi, ku wapi kushinda kwako? Lakini Mungu na ashukuriwe, anayetupa ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” Naam, bwana.

Ilikuwa ni kitu gani? Mungu alijinyenyekeza. Loo!

246 Wakati mwanadamu alipotenda dhambi, alivuka shimo kubwa lililowekwa kati yake na Mungu, akawa hana njia ya kurudi. Na ndipo Mungu akachukua kabadala, akatoa dhabihu ya kabadala, na akakikubali. Basi kama mwanadamu angekubali kabadala hiki mahali pake, basi angeweza kuvuka aingie katika ushirika pamoja na Mungu, kama nilivyosema hapo mwanzo. Na basi wanadamu, kwa miaka mingi, walishughulika kwa damu ya mbuzi, na kondoo, na wanyama. Hawangeweza kamwe kuondoa dhambi. Ilifunika tu dhambi.

247 Lakini basi ni jambo gani lilitukia? Ilikuwaje? Siku moja kulitokea kitu fulani ambacho kiliweza kuondoa dhambi, Damu ya Mwanawe. Naye aliondoa dhambi.

248 Sasa, hapa si muda mrefu uliopita . . . Sasa, sitajua. Huenda kukawa na wanasayansi walioketi hapa. Nitatoa tamshi. Nitaliita tu ni kitu fulani. Halimaanishi hicho, hata kidogo. Lakini nitasema, tulikuwa tukinini . . . Tunapata, kama vile tone moja dogo, la kawaida la wino. Mungu anaweza kujificha katika hilo. Unaona? Kama ni tone la wino, ilibidi liwe ni kitu fulani kabla halijakuwa tone la wino. Hebu na tuone lina nini.

249 Kwanza, ni tone, wino. Ni kitu gani? Ni kemikali. Hebu tulivunje kulirudisha nyuma. Lilitoka wapi? “Vema,” unasema,

“basi, kutoka kwenye maji yake.” Hayo ni H₂O, fomyula fulani. Hiyo ni sehemu yake.

²⁵⁰ Halafu lina kemikali fulani ndani yake, ya rangi. Rangi hiyo ilitoka wapi? Sasa, kuna rangi moja tu ya asili, na hiyo ni nyeupe. Tunajua jambo hilo. Rangi nyingine zote zimetengenezwa kutokana na nyeupe. Kwa hiyo basi, tunaona, ilipataje kuja? Hii ilitoka wapi?

²⁵¹ Sasa hebu na tuifuatilie kule nyuma. Jambo la kwanza unajua, “Vema, vema,” unasema, “inakuwa asidi.”

²⁵² Kutoka kwenye asidi, ndipo inakuwa nini? Jambo linalofuata, inarudi, “Vema,” unasema, “basi inatoka kutoka kwenye nu—nuru fulani.” Nuru ni kitu gani? Inakuwa molekuli nyingi sana.

²⁵³ Na sasa hebu na tuseme molekuli moja, molekuli nne, molekuli nane, zinaungana, na kufanya atomu moja, mara atomu nne, mara atomu sita. Sasa, kama ingekuwa ni atomu nne mara atomu tano, ingekuwa ni *nyeupe*. Ilitokea kuwa ni sita. Ni kitu gani kiliamua jambo hilo? Wapi ninaunganisha kemikali, pamoja, kufanyiza rangi hiyo, wino mweusi? Unaona? Vema.

²⁵⁴ Yote ilitengenezwa. Basi ilitoka wapi? Ilibidi itoke mahali pengine. Ilibidi itoke kwa Muumba, kwa maana ni uumbaji. Uumbaji hauna budi kutoka kwa Muumba.

²⁵⁵ Kwa hiyo basi inakuwa wino. Ulikuwa ni kwa kusudi fulani. Unaweza kuandika msamaha wako. Ungeweza kuandika Yohana 3:16 na kuokoa nafsi yako. Na basi, pia, ungeweza kuandika hukumu yako, na ikupeleke kwenye kizimba cha mauti. Uko hapa kwa kusudi fulani.

²⁵⁶ Sasa, miaka hii yote umekuwa vile ulivyokuwa, ukiwa umeamuliwa na kitu fulani, upate kufanywa kile ulicho. Sasa utawezaje kuurudisha kule nyuma?

²⁵⁷ Walitengeneza kitu kinachoitwa dawa ya madoa. Ninyi wanawake mnaitumia, Kloroksi. Sasa, nina beseni la Kloroksi lililowekwa hapa, nami ninadondosha hilo tone la wino katika ndoo hiyo ya Kloroksi. Sasa tafuta rangi yako. Nini kimetokea kwa rangi hiyo? Imekuwaje? Jambo la kwanza ililofanya, iliingia majini, ikadondokea kwenye Kloroksi. Kemikali hiyo ilikuwa na nguvu sana mpaka ikairudisha huko nyuma kabisa. Huwezi kuona mvuke wowote wake wala chochote kile. Imetoweka. Haitakuwako tena, kwa sababu imerudi mahali pa asili ilikotoka.

²⁵⁸ Na sasa hivyo ndivyo ambavyo hasa Damu ya Yesu inavyoifanya dhambi. Damu ya Yesu Kristo! Kiri dhambi yako kwenye Damu ya Yesu Kristo. Inafuta. Inazitupa katika Bahari ya Usahaulifu, wala hazitakumbukwa tena dhidi yako, hata kidogo.

259 Sasa, Kanisa liko wapi siku hizi, ndugu, kama tumezaliwa kuwa wana wa Mungu?

260 Na Yesu Mwenyewe alisema, “Kama sheria yenu wenyewe ilisema ninyi ni ‘miungu,’” miungu wadogo wanaoitawala dunia. Yeye alisema, “Kama wanawaita hao ‘miungu,’ ambao walijiliwa na Neno la Mungu,” ambao walikuwa ni manabii. Neno la Bwana humjia nabii. “Na kama mnawaita ‘miungu,’ mnanihukumuje,” akasema, “ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?”

261 Sasa, kama damu ya mafahali na mbuzi iliweza kumpa Musa nguvu, atoke aende kule, kwa agizo la Mungu, na kunyosha ile fimbo, na kusema, “Na kuje nzi.” Yeye alikuwa na Neno la Mungu, naye alilineni Neno hilo. Na wakati alipofanya hivyo, lilitoka kwenye wazo la Mungu. Neno ni wazo lililotamkwa. Na kwa hiyo basi wakati Mungu alipoliwazia, na kuliweka moyoni mwa Musa, naye akalinena, liligeuka likawa Neno. Ndipo Musa akageuka na kurudi; labda hakuna hata nzi mmoja nchini. Katika saa moja tokea wakati huo, labda maskini nzi mmoja wa kijani kibichi alianza kuvuma hapo. Katika nusu saa, kulikuwa na ratili kumi kwa yadi moja mraba. Kilikuwa ni kitu gani? Neno la uumbaji la Mungu lililonenwa kwa midomo ya mwanadamu.

262 Mungu hutumia wanadamu. Mungu angeliweza kutumia jua kuhubiri Injili. Mungu angeliweza kutumia upepo kuhubiri Injili. Bali Mungu aliwachagua wanadamu kuihubiri Injili.

263 Kanisa lina shida gani siku hizi? Kuna kasoro fulani. Maoni yangu, hatuji na ule uaminifu, kwenye jambo sahihi, kwa ajili ya jambo hilo. Kama Mungu angeweza kufanya jambo hilo kwa damu ya fahali, mbuzi na mafahali ambayo ilifunika tu dhambi na kufanya upatanisho kwa ajili ya mwenye dhambi, bali dhambi bado ingali ilikuwapo (ila tu imefunikwa), Yeye anaweza kufanya nini kwa Damu ya Mwanawe ambayo huondoa dhambi? Na Mungu hakutengeneza, bali aliumba Damu inayoondoa dhambi yote.

264 Na Marko 11:24, “Lolote utakalouambia mlima huu, ‘ng’oka,’ wala usitie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Kanisa la Kipentekoste liko wapi, leo? Amina. Hutambui ya kwamba iliyotubiwa, dhambi iliyotubiwa kweli, huondoa dhambi. Kama haiondolewi. . . Inajenga daraja la kuvuka shimo kubwa, jambo hilo linamrudisha mwanadamu katika Uwepo wa Muumba Wake na kumfanya mwana wa Mungu. Amina. “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Amina. Haya basi. “Amin nawaambia, ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale ambayo umesema yatatimia, yatakuwa yako.” Utukufu kwa Mungu. Ni Mungu wangu akijifunua Mwenyewe katika unyenyekevu. Unaona?

265 Mungu akimchukua mwenye dhambi mnyenyekevu na kumsafisha kwa Damu Yake, na kuidondosha dhambi iliyotubiwa katika Kloroksi-takasi ya Damu ya Mwana wa Mungu, na kuweka Uhai Wake Mwenyewe katika mtu huyo, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ndipo basi kama tuna ubatizo halisi wa Roho Mtakatifu, tuna shida gani sisi? Wakati, ule mfano, wakati Eliya alipoangusha lile joho kwa ajili ya Elisha, alipata sehemu maradufu yake. Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Na kuu kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi ninaenda kwa Baba Yangu.” Kuna shida gani, enyi kanisa?

266 Sasa, mmetuita sisi ni Beelzebuli, juu ya maono na vitu kama hivyo. Ondokeni nyuma yangu. Ndugu, shuka uende msalabani. Iendee Injili. Si lazima tuige. Kwa nini uchukue uigaji? Kwa nini uchukue wazo la uongo la jambo Hilo? Wakati, mbingu zimejaa nguvu halisi za Kipentekoste ambazo zinamfanya mwanamume ama mwanamke, mwana au binti ya Mungu, zinazomrudisha kwenye Uwepo wa Mungu. Amina. Haya basi, Mungu akijifunua Mwenyewe katika unyenyekevu.

267 Inakupasa kutoka kwenye mawazo yako mwenyewe. Inakupasa kuruhusu nia iliyokuwa katika Kristo iwe ndani yako. Inakupasa kudumu pale mpaka kila dhambi ya uoga, kila dhambi ya mashaka imetoka moyoni mwako. Na kama uko hapo, na Mungu hakuchukui na kukuondolea dhambi zako na kukupeleka kwenye Uwepo wa Mungu, tukio lako lina kasoro.

268 Sijali una digrii ngapi za udaktari, una kanisa kubwa jinsi gani, kwamba wewe uko chini ya ushawishi wa shirika kubwa jinsi gani, kwamba ni madhehebu mangapi, chochote kile, hakina uhusiano wowote na jambo hilo, mpaka dhambi zako zimetubiwa na zimo katika Damu ya Yesu Kristo. Mtu unasimama kama mwana na binti wa Mungu aliye safi na aliyezaliwa mara ya pili, ukiwa na Uzima wa Mungu ndani yako, kunena Neno la uumbaji, “Mlima huu na ungoke,” na utakutii. Amina.

269 Mungu akijifunua Mwenyewe katika unyenyekevu. Yeye huwachukua watu wa aina hiyo wasio na elimu. Anawachukua hao wa aina hiyo ambao wataamini tu jambo hilo. “Ninakushukuru, Baba, Muumba wa mbingu na nchi, umewaficha mambo haya wenye hekima na akili.”

270 [Sehemu tupu ya kanda—Mh.] “. . . alipigwa na kujeruhiwa. Na hata hivyo tulimhesabu kwamba amepigwa na kujeruhiwa, hakika, na Mungu. Bali alijeruhiwa kwa ajili ya makosa yetu.” Ile Kloroksi ilikuja. “Alichubuliwa kwa makosa yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake. Na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.”

271 Yeye alifanya nini? Alijidhili hata kufa, kwenye alasiri ya Ijumaa kuu, apate kufufuka Jumapili ya Pasaka, amina, apate

kumtuma Roho Mtakatifu juu ya Kanisa, pamoja na sehemu maradufu Yake, tupate kufanya mambo yale anayofanya, ambayo alifanya. Yeye aliahidi, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Na jinsi tunavyoenda mbali Naye, kwa mapokeo yetu! Haya basi.

²⁷² Mungu akijificha katika unyenyekevu, akijifunua Mwenyewe katika nguvu, hivyo ndivyo Mungu anavyofanya jambo hilo. Huo ndio mpango wa Mungu wa kufanya jambo hilo, naam, bwana, apate kuwaleta wana wavuke shimo hili.

²⁷³ Katika kufunga, pengine niseme jambo hili. Mungu akijificha katika mauti, apate kuja tena katika ufufuo. Ninataka kuwaambia hadithi ndogo niliyosoma si muda mrefu uliopita, katika kufunga. Wao walisema. . .

²⁷⁴ Katika wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia, baba zangu wakubwa walikuwa huko. Binamu zangu walikuwa kwenye vita hivyo. Wengi wao waliuawa.

²⁷⁵ Lakini katika sehemu moja, basi, walikuwa na rejimenti n—zima ya askari wa Kimarekani, waliozingirwa. Jeshi la Kijerumani lilikuwa limewazingira. Na risasi za bunduki za rasharasha, na mizinga mikubwa, na chochote walichokuwa nacho, na kutupa risasi za makombora, chochote kile, viliwafanya wazingirwe. Wasingeweza kutoka, wala hakuna njia ya kutoka.

²⁷⁶ Hiyo hapo rejimenti nzima ya askari wanaoangamia papo hapo, kwa sababu wao walikuwa kila upande. Walikuwa na ndege. Wasingethubutu kurusha moja; ingetunguliwa. Mtu akijaribu kutoroka; vema, wao, waliwazingira tu kila upande. Hakukuwa na chochote. Bunduki zao nzuri zilikuwa zimeshindwa. Mbinu zao zote za kijeshi zilikuwa zimeshindwa. Walikuwa wamezingirwa na adui. Hapakuwapo na njia ya kutokea. Hapakuwapo na kitu chochote.

²⁷⁷ Ndipo, hatimaye, maskini askari mmoja akajitokeza. Alipata ufumbuzi wa njiwa, moja ya hao njiwa wa nyumbani. Hilo lilikuwa ndilo tumaini lao pekee. Wakaandika ujumbe, na wakawazia, “Laiti njiwa huyu angefanikiwa kupita, na arudi kwenye makao makuu ambako alitoka, anaweza kuuchukua ujumbe huu.” Njiwa wa ujumbe, njiwa mjumbe, na hicho kilikuwa ndicho kitu pekee walichokuwa nacho: njiwa mdogo, wa kawaida. Zana zao zote zilikuwa zimeshindwa. Bali walikuwa na njiwa mdogo, wa kawaida. Wakaandika huo ujumbe na kuufunga kwenye maskini mguu wake mdogo, kisha wakamwachilia aende, kwa baraka na maombi, kwamba apate kufaulu.

²⁷⁸ Hapana budi, Wajerumani walimwona huyo njiwa mweupe akipaa juu. Wakamfyatulia risasi, na chochote kile. Risasi moja ikapitia kwenye bawa lake, ikamnyofoa manyoya. Nyingine ikamkwaruza shingoni, ikakata tumbo lake. Nyingine ikapiga

mguu wake uliokuwa na ule ujumbe. Bali maskini njiwa huyo mdogo aliendelea kuruka, akijitahidi kuufikisha ujumbe. Hana budi kuupeleka. Maisha yalikuwa hatarini. Hatimaye, kwa jitihada zake, na kuyumbayumba hewani, na kugeuka, na kuruka, kisha akaanguka. Ndipo akaangukia kwenye kambi ya jeshi, ama kambini mahali walipokuwa wale askari.

279 Askari mmoja akamwokota, akamwangalia. Maskini jamaa huyo akasema, “amepigwa risasi.” Akafungua, akaangalia mguu wake mdogo, kwenye mguu wake mdogo uliojeruhiwa, na kulikuwa na ba—barua. Wakasoma hiyo barua. Ilikuwa imejaa damu. Ingawa ilikuwa imejaa damu, huo ujumbe ulifika. Ulifika. Wakatuma askari wa kuongezea nguvu, upesi, na kuokoa rejimenti nzima ya askari. Kama maskini njiwa huyo mdogo asingefanikiwa, hao watu wote wangaliangamia. Huo ungekuwa ni msiba wa jinsi gani! Ingekuwa ni maafa ya kutisha. Na hilo lilikuwa ni jambo kubwa kwa huyo njiwa mdogo kufanya, ingawa lilifanya damu yake imwagike. Damu yake ilikuwa kwenye huo ujumbe.

280 Hilo lilikuwa ni jambo kubwa, lakini halikufikia nusu yake, hata siku moja wakati dhambi ilipokuwa imewazingira wana wa Mungu. Hapakuwapo na matumaini. Hakukuwa na kitu wangeliveza kufanya. Matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Lakini palikuja, si njiwa mdogo, bali Hua. Miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, alasiri hii, katika urahisi, alikuwa amezaliwa horini, akifa msalabani, bali alifika Mbinguni akiwa na Damu Yake Mwenyewe iliyokuwa kwenye huo Ujumbe. Naye akawakomboa wana wa Mungu, kwamba sasa tunaweza kuwa tena wana wa Mungu na binti za Mungu, kuishi katika utakatifu na usafi, kuishi katika Uwepo Wake. Ninashukuru sana kwa ajili ya Hua huyo aliyeshuka kutoka Utukufuni, aliyechukua Ujumbe, ya kwamba, nilikuwa mhitaji, Naye akaruka akaenda Mbinguni Nao. Na ulikuwa na damu, kila mahali, yale ambayo dhambi za ulimwengu zilikuwa zimetenda. Lakini, leo, nimewekwa huru. Niko huru. Nina furaha sana.

281 Na, hata hivyo, watu wanyofu wanaweza kufahamu jambo Hilo. Nina furaha mimi ni mtu wa kawaida kutosha kuweza kulifahamu. Je! hamna furaha kwa ajili ya jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hivi hamna shukrani? [“Amina.”] Mungu akijificha Mwenyewe katika urahisi.

282 “Yeye alihesabiwa na akadharauliwa. Tulumhesabu amedharauliwa na kuteswa. Tulificha, kusema kweli, uso wetu Kwake.” Hakuwa huyo askari mkuu waliyedhani angekuwa. Hakuwa askari hodari waliyekuwa wakimtaamia. “Lakini waliuficha uso wao Kwake.” Waliona haya. “Lakini, hata hivyo, alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu.” Ilikuwa ni nini? Mungu akijificha katika urahisi. Yehova akifanyika Mtu, apate kufa kwa ajili ya wanadamu; apate

kuurudisha Ujumbe, kwa Damu Yake Mwenyewe, masharti ya Mungu, ya kwamba ile gharama ililipwa, nasi tumekombolewa.

²⁸³ Na leo, ingawa ni jambo la unyenyekevu namna hiyo, haikulazimu kuwa mwerevu, haikulazimu kuwa na elimu. Amini tu huo Ujumbe, Neno la Mungu. Nawe pia unaweza kuokolewa na uwe Mwana wa Mungu, uweze kusimama katika Uwepo wa Mungu, na kufanya kazi za Mungu.

²⁸⁴ Na tuinamishe vichwa vyetu kidogo tunapoomba baraka za Mungu juu ya mambo haya.

²⁸⁵ Ninataka kuwauliza jambo fulani. Leo, kama vile redio zilivyoendelea, na magazeti. Niliona gazeti asubuhi ya leo, mahali ambapo walikuwa wakionyesha igizo fulani, mtu fulani akiubeba msalaba. Wana kila aina ya mambo. Kwenye asubuhi ya Pasaka, kanisa zima litapambwa kwa mayungiyungi. Madhabahu zitajazwa mayungiyungi. Sungura wa Pasaka akiwapo, kuku, sijui hayo yana uhusiano gani na Pasaka. Sungura, mnyama mchafu, mbele za Mungu, hata walikatazwa kuwala au kuwagusa katika wakati wa Biblia. Na kuku, jambo lile lile, mabata. Lakini hata hivyo kilichukua mahali pa kufufuka. Baba Kristmas alichukua mahali pa Krismasi. Loo, jamani! Ulimwengu umefikia wapi, ewe rafiki? Tuko wapi? Unaona mahali ambako tumeenda? Tunaelekea moja kwa moja kwenye shimo. Hiyo ni kweli. Tumbanwa na dhambi, na kanuni za imani na mafundisho ya sharti.

²⁸⁶ Lakini Mjumbe alivuka, miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, alasiri hii. Masharti yalitimizwa. “Mwana wa Mungu, aliyefanyika katika mfano wa mwili wenye dhambi, aliyezaliwa katika hori. Hana uzuri hata tumtamani. Alikuwa ni mtu wa kushutumiwa. Hatukumtamani. Tulimficha nyuso zetu.” Tungali tunafanya jambo lile lile leo.

Unasema, “Nisingelifanya jambo hilo.”

²⁸⁷ Loo, msimamo wako leo unathibitisha ungalilifanya. Unalifanya sasa. Unaona? Kwa nini usichukue njia ya unyenyekevu? Useme, “Bwana Mungu, sijali itanigharimu nini. Sijali ni kitu gani. Nimemalizana na dhambi.” Si—sisemi wewe ni mbaya, sisemi unavuta sigara, unakunywa pombe, wala chochote kile. Bali huamini Neno. Unaona?

²⁸⁸ Kama unaamini Neno, basi useme, “Bwana, sijali inanigharimu nini. Ikinigharimu dhehebu langu, kama ikinigharimu karamu yangu ya kushona, kama ikinigharimu chama changu, kama ikinigharimu sifa miongoni mwa rafiki zangu, sijali itanigharimu nini. Nitakubali ujumbe wa Kalvari. Nitakuwa mnyenyekevu. Nitajinyenyekeza, tangu sasa na kuendelea.

²⁸⁹ “Ninajua, kama nikiacha nywele zangu zikue,” ninyi wanawake, “wataniita wa mtindo wa kale. Sijali wataniita nini. Nitakuwa mama mwenye heshima. Wananiambia ninaonekana

kama nimepauka na nimekufa. Nimekufa katika Kristo. Nitafanya jambo hilo.”

²⁹⁰ Wanaume, “Sijali wanajaribu kunishindilia mafundisho mangapi ya sharti na kanuni ngapi za imani. Tangu sasa na kuendelea, ninaukubali Ujumbe mnyenyekevu wa Mungu. Nitauamini. Nitakaa pale mpaka dhambi zangu zimeondolewa. Nitakaa hapo mpaka Roho Mtakatifu ajimimine ndani yangu, imani kwa kila Neno la Mungu lililoandikwa. Yeye aliniahidi jambo Hilo. Na kama nina shimo lile la kuvuka pale, daraja, kwa Damu Yake yenye haki, basi ninaweza kusimama kama mwana wa Mungu. Ninaamini Injili yote. Nitafanya hivyo.

²⁹¹ Je! ungependa kufanya hivyo? Je! ungependa huko kujiweka wakfu sasa hivi? Kama ungependa, inua mkono wako kwa Mungu. Na useme, “Nikumbuke, Ndugu Branham, unapoomba. Ninataka Mungu afanye jambo hilo.” Mungu akubariki. Ni kweli. Vema. Yeye anaona mkono wako.

²⁹² Baba yetu wa Mbinguni, unyenyekevu, unyenyekevu wa kukuamini Wewe, jinsi unavyojifunua Mwenyewe katika unyenyekevu! Jinsi ambavyo tunaona katika siku hizi, na siku zote, ya kwamba kanisa litajiingiza katika hali hiyo. Ndipo utainama moja kwa moja, kwenye hilo shimo refu kutoka mahali pasipojulikana, na kuokota kitu fulani, kukitia mafuta, kukituma, na kitakataliwa, kisha unauhukumu ulimwengu kwa jambo hilo.

²⁹³ Mungu, tunaona siku hizi, ya kwamba, kwa miaka hamsini, Roho Mtakatifu wa thamani, ambaye watu wamejaribu kumkubali kupitia kwenye mafundisho ya sharti, na hata hivyo ulimleta katika nguvu Zake na dhihirisho Lake. Kundi nyenyekevu la watu maskini, waliokataliwa waliodharauliwa wakamkubali, wakamwamini. Umejitukuza ndani yao, Bwana. Na sasa tunawaona, katika kizazi kingine, wakijaribu kufanyika wajukuu kwa Mungu. Ee Mungu, ni jambo la kuchukiza jinsi gani! Jalia wanaume na wanawake wakimbilie upesi kwenye unyenyekevu wa kuiamini injili. Tujalie, hilo, Bwana.

²⁹⁴ Mikono mingi iliinuliwa hapa, usiku wa leo, wanaume wengi na wanawake. Na, Bwana Mungu, ninaomba ya kwamba utawabariki. Ninaomba ya kwamba usiku uu huu watapata amani ya Mungu katika kila mmoja wa mioyo yao; hivi kwamba watajazwa tele na Roho Wako, hivi kwamba watapata imani kufanya miujiza, imani ya kuishi maisha ya kitauwa; kuishi maisha matamu sana, hivi kwamba, watakaponenwa vibaya, hawatarudisha mabaya; kwamba wanaweza kurudisha busu kwa kofi; kwamba wanaweza kurudisha mema kwa mabaya. Tujalie hilo, bwana. Wafanye wanaume wawe wanyenyekevu. Wafanye watu wapate kukujua Wewe katika Nguvu za kufufuka Kwako. Jalia mauti Yako yasiwe bure kwetu sisi katika kizazi hiki.

²⁹⁵ Tunaomba sasa ya kwamba utaliinua Kanisa Lako, Bwana. Litukuze na ulikuze. Lipeleke nyumbani kwenye Utukufu, Tunaamini mambo haya, Baba. Wafanye wengi hapa, usiku wa leo, wanaomtafuta Mungu, wampate katika saa hii. Tunaomba haya katika Jina la Yesu.

Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

²⁹⁶ Sijui sasa kama mngependa kupiga hatua nyingine kuelekea kwenye jambo hilo, kama mnetaka kusimama na kusema, “Sioni haya, ingawa mimi ni mfuasi wa kanisa. Mimi ni Mmethodisti, Mbatisti, ama Mpentekoste,” hata uwe nani. “Sioni haya. Ninatambua ya kwamba nimetegemea sana mambo yale nijuayo. Bali kamwe sijafika mahali ambapo ningeweza kuamini kikamilifu Injili yote, na kuifanya ifanye kazi maishani mwangu. Nimeona mambo. Ninaamini hizo ni ahadi. Ninataka kuziamini. Lakini Yeye aliniambia, kama niliamini jambo Hilo, jambo *hili* lingetendeka. Kwa hiyo, kuna kasoro kwangu. Halifanyi kazi. Nilijaribu kulifanya lifanye kazi, bali halifanyi kazi. Nami ninalionea aibu. Nami ninataka ulimwengu ujue, ninataka watu waliopo hapa wajue, ya kwamba mimi ni mwaminifu na ninalitaka maishani mwangu. Ninataka kuwa shahidi mwaminifu kwa ajili ya Kristo, huku Injili yote ikijidhihirisha yakini maishani mwangu.” Je! utasimama kwa miguu yako na kusema, “Ninataka kuwa shahidi kwamba ninamtafuta Mungu”? Mungu awabariki. Naam. Unaona?

Yesu alisema, “Kama unanionea aibu mbele za watu, nitakuonea aibu mbele ya Baba Yangu.”

²⁹⁷ Sasa, kama watu hawa ambao ni Wapentekoste, ama Wamethodisti, ama Wabaptisti, je! wana mambo haya ya kweli, kama umevuka shimo hilo refu sana, mpaka utakapojua yakini ya kwamba umesimama Mbele ya Mungu, mwana ama binti wa Mungu aliyekombolewa? Na ishara na maajabu, si jambo la kujifanya kuamini, bali chombo halisi cha Mungu. Roho Mtakatifu, anawaka ndani yako? Na yale uuambaiyo mlima huu, unang’oka? Unaamini jambo hilo? Usipong’oka, sasa ndio wakati wako.

²⁹⁸ “Unajua je ya kwamba ni ninii yangu . . .” Unasema, “Vema, nilisimama huko nyuma.”

²⁹⁹ Vema, kama wewe una njaa kweli ya Mungu, utaendelea kusimama mpaka Hiyo itakapokuja. Hakuna mwisho wake. Wewe unang’ang’ania. Kama yule mwanamke Msirofoinike, asingeweza kuchukua “la.” Aliutaka, kweli. Je! uko tayari kusimama? Kuna mwingine zaidi kabla hatujaomba? Ule wimbo mzuri:

Aligongelewa misumari msalabani kwa ajili
yangu;
Msalabani alisulibishwa, hapo akafa kwa ajili
yangu.

300 “Ninamtaka Huyo, Ndugu Branham. Ninamtaka, Mungu. Kweli ninamtaka. Maisha yangu, vema, ninataka kubadilika. Nime—nimeishi kwa kubahatisha. Nimeishi kwa kutumainia. Ninataka kitu fulani. Ni—ninataka. Kama hao mitume waliweza kulenga hiyo alama ya sufuri, kila wakati, nami pia ninaweza.”

301 Hivyo ndivyo ninavyosema. Kama lilifanya kazi kwa mitume, linafanya kazi sasa. Kama lilitukia wakati mmoja, linatukia tena. Kama Yeye alipata kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. “Ni yeye yule jana, leo na hata milele.” Hilo ndilo neno langu la kampeni. Kama dhehebu lako haliadini jambo hilo, acha madhehebu yako yaadini yanavyotaka. Wewe amini Biblia. Iadini. Je! ungetaka kusimama? Kama wanane ama kumi zaidi walisimama wakati huo. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Wengine zaidi wanasimama, wengine zaidi wanasimama. “Mimi kwa kweli ninamaanisha, Ndugu Branham. Ninamtaka.”

302 Jambo fulani lilitukia hivi majuzi. Mlisoma, ama mlisikia ile kanda, “zile ngurumo saba” *Je! Bwana, Ni Wakati Gani?* Unaona? Jambo hilo lilitukia hivi majuzi. Mnajua mambo haya. Wakati umewadia, enyi kanisa. Wakati umewadia. Msi-, msi-, msingojee muda mwingine zaidi. Unaona?

303 Unajuaje kwamba kunyakuliwa hakuendelei kutendeka wakati wote? Muda si muda unajua, kutakuwa kumepita, mmoja akitoweka *hapa* na *pale*. Kutakuwa kumekwisha pita, unajua, muda si muda. Nanyi mtaninii...Hukumu itaupiga ulimwengu. Unasema, “Vema, ni—nilifikiri *hivi*.” “Muda umeenda sana sasa.”

304 Kumbukeni, hawakujua jambo hilo mpaka ile siku waliyoingia katika safina, ndipo wakawa wamechelewa sana. Huyu mwanamwali mpumbavu hakuajua mpaka aliporudi na akakuta mwanamwali mwerevu ameondoka, ndipo akawa ameachwa kwa kile kipindi cha Dhiki.

305 Hakuna mwalimu mzuri anayeamini ya kwamba kanisa, Bibi-arusi...Kanisa linapitia kwenye ile Dhiki, bali si Bibi-arusi. Kanisa linapitia, kwa ajili ya utakaso, hakika, chini ya muhuri wa sita. Naam. Israeli inapitia kwenye jambo lile lile, kwa ajili ya wale mia moja na arobaini na nne elfu, bali si Bibi-arusi. Kuna...

306 Bibi-arusi amesamehewa. Anaenda moja kwa moja Utukufuni, katika Unyakuo. Hiyo ni kweli. Yeye, kwa maoni yangu, mtu wa mwisho atanyakuliwa, moja ya siku hizi. Huenda ikatokea, nawe usingejua kitu juu yake. Kumbuka, ni siri, kunyakuliwa kwa siri. “Yeye atakuja katika wakati usiutarajia.” Hutajua kitu juu ya jambo hilo. Atakuwa ametoweka; itakuwa imechelewa sana wakati huo.

307 Unasema, “Laiti ningalisimama.” Kama kamwe ulitarajia kufanya uamuzi, hebu mkutano huu, hapa Albuquerque, hebu huu uwe ndio wakati ambapo ulifanya maamuzi.

308 Sasa, kama ukijisikia uko salama kweli kwa ajili ya Kristo, unajisikia ya kwamba una Roho Mtakatifu na Damu ya Yesu Kristo, ishara zote na ahadi ziko chini ya amri yako, na unazona zikidhihirishwa na zikifanya kazi maishani mwako, na unajua kwamba ni za kweli; kama umeketi hapo namna hiyo, na unaamini jambo hilo, nitaamini unayosema. Hiyo ni juu yako. Kama siyo ulivyo, unapaswa kusimama kwa miguu yako. Lakini kama unaamini jambo hilo, na unajua ya kwamba ishara hizo na maaajabu ambayo Yesu, uthibitisho wa Masihi, unanena na wewe; kama siyo, basi unapaswa kusimama kwa miguu yako. Mbarikiwe. Hiyo ni kweli.

309 Mimi ni mgeni kwa wengi wenu. Wengi wenu wamenichukua kama mwonaji. Sijasema kitu juu ya jambo hilo. Mnajua hilo. Nimenyama-... Saa hiyo haijawadia bado. Lakini mnaniamini sasa. Mnaniamini, kama mtumishi wa Mungu. Je! nimepata kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana isipokuwa lile lililotimia? Kama ndivyo ilivyo, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Halijakosea hata, kwa maelfu ya mambo, halijawahi hata siku moja bali daima limekuwa ni kweli. Mnajua jambo hilo, kote ulimwenguni.

310 Ingawaje, hamkubaliani nami, wengi, katika teolojia. Wala mimi si mwanateolojia. Ninasema tu yale ninayoyasikia. Na basi wakati ninaposikia jambo, ninaangalia katika Biblia. Kama halilingani na Biblia, nisingelipokea. Lakini hakuna hata wakati mmoja yamepata kuwa kinyume na Neno, bali yamekubaliwa na Neno. Hiyo ndiyo sababu yamethibitishwa. Mungu anayathibitisha.

311 Sasa, nisikieni, basi. Kama mnaniamini mimi kwamba ni m—mjumbe aliyetumwa kutoka kwa Kristo, kwenu, niaminini. Kama hamko katika Ufalme wa Mungu, afadhali mwingie haraka.

312 Hali haitakuwa nafuu. Itazidi kuwa mbaya, sikuzote. Sasa hebu andikeni jambo hilo. Unaona? Kumbukeni tu, angalieni mwone kama jambo hilo ni kweli ama si kweli. Angalieni kama litakuwa ni kweli ama si kweli. Mambo hayatakuwa nafuu. Yataendelea kuwa mabaya zaidi. Mambo yatazidi kuwa magumu, wakati wote. Uamsho umekwisha. Mnakusanya masazo tu ya mashamba. Umekwisha. Sasa mnasema, "Sikubaliani na jambo hilo." Sawa. Ni sawa, kama hamkubaliani. Hilo ni sawa. Hiyo ni imani yangu. Hayo ndiyo nisikiayo kutoka Mbinguni.

313 Ninaamini wakati wa Laodikia ndio wakati wa Kipentekoste, ambapo inafikia mahali pa uvuguvugu, ndipo Mungu analitapika litoke kinywani Mwake. Na hapo ndipo limefikia sasa hivi. Uamsho wa Kipentekoste umefikia mahali hapo, vuguvugu, si moto sana, si baridi kama barafu. Hamko

baridi na wa kawaida, wala hamko moto. Mko katika hatua ya kutapikwa, na mtatapikwa.

³¹⁴ Yesu, wakati pekee aliopata kusimama nje ya kanisa. Mafundisho yao ya sharti yalikuwa yamemtoa nje. [Ndugu Branham anagonga mimbara—Mh.] Akibisha, akijaribu kurudi mlangoni, “Tazama, ninasimama mlangoni, na nabisha; kama mtu akisikia Sauti Yangu...” Ninafuraha mmesikia, usiku wa leo.

Sasa, Ninaweza tu kuwaomba msimame.

³¹⁵ Yeye anakuangalia. Yesu alisema, ya kwamba, “Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, Nipo papo hapo katikati yao.” Kama hiyo siyo kweli, hakuna Mungu; hakuna Biblia; hakuna kuchomoza kwa jua; hakuna kutua kwa jua; hakuna maua; hakuna mti; kwa kweli wewe huko hapa; uko katika ndoto; maisha si halisi; wewe si mwanadamu. Kwa hiyo, hilo haliwezekani kuwa hivyo, kwa hiyo haiwezekani Kwake kutokuwa hapa. “Na kama mtaomba lolote katika Jina Langu, mkiwa na imani ya kuamini, Yeye atawapa.”

³¹⁶ Sasa, huyo ni wewe sasa. Ulisimama kama shahidi, ya kwamba unamtaka. Sasa, katika njia yako mwenyewe, jinsi unavyoomba, jinsi unavyotaka, ninataka useme, “Bwana Mungu,” moyoni mwako. Sasa usisikilize kitu. . . U—u—uamsho huu hapa utakupa wakati mwingi kwa ajili ya jambo hili, wakati wote unaotaka. [Ndugu mmoja jukwaani anasema, “Naam. Hiyo ni kweli.”—Mh.]

³¹⁷ Sasa, katika njia yako mwenyewe, katika njia yako mwenyewe. Sasa, ninajua ni jambo la kawaida kwamba mtu mmoja husimama, huyo mwingine anasimama, hao wengine anapiga magoti *hivi*. Lakini vyovyote mnavyotaka, sijali ni kitu gani. Usiseme, “Bwana, jalia nifanye *hivi*. Jalia nifanye *vile*.” Sema tu, “Bwana, nijaze. Nijaze na Roho Mtakatifu. Hili linatoka moyoni mwangu kabisa. Ninamaanisha.” Sasa, kama kweli unalimaanisha, hana budi kuja. Haiwezekani asije. Yeye aliahidi, Naye anakazana kuingia moyoni mwako.

³¹⁸ Jambo pekee, uliufungua kidogo tu, na kusema, “Njoo ndani na usimame *hapa*, lakini usizunguke huku na huko, usijishughulishe na maisha yangu ya binafsi.” Unaona?

³¹⁹ Yeye anakutaka wewe. Anataka yote uliyo. Anataka kila sehemu ya moyo wako. Anataka maisha yako binafsi. Anataka maisha yako yote. Anataka kuwa Bwana Wako. *Bwana* ni “umilikaji.” Yeye anataka kukumiliki, kusudi apate kukuongoza, kukuelekeza, kukuchukua, kukutumia. Je! uko tayari kufanya jambo hilo? Kama uko tayari, Yeye anataka kuingia ndani, la sivyo usingekuwa umesimama pale. Unaona? Kwa hiyo sasa ndio wakati wako wa Kulipokea.

³²⁰ Sasa ni juu yako. Sasa, kama utaamini kwa moyo wako wote, litatatuliwa tangu sasa. Huu utakuwa ni usiku wa kukumbukwa.

Labda hawatafunga milango hii usiku wa leo. Utakaa usiku kucha hapa. Lakini kama unataka jambo hili kweli, sema, “Bwana, ninasimama kwa miguu yangu. Mpaka utakaponijaza kulingana na ahadi Yako, sitasogea kamwe kutoka mahali ninaposimama.” Kuwa makini na Mungu, Yeye atamaanisha kabisa na wewe.

³²¹ Lakini mpaka utakapofanya jambo hilo, unagonga, “Bwana, utanipa Roho Mtakatifu usiku wa leo? Sisikii kitu. Vema, labda nitajaribu kesho usiku.” Hutapata kitu chochote kutoka kwa Mungu, namna hiyo.

³²² Huna budi kuja, umedhikika, ukifa, ndipo unampata. Hiyo ni kweli. Yeye alitoa ahadi. Kama sivyo, kwa nini upoteze wakati wako, kama ahadi hizo si za kweli?

³²³ Hivyo ndivyo mambo haya yanavyotendeka. Hiyo ndiyo sababu mimi naweza kusimama na kuuambia ulimwengu, “Je! Neno limewahi kukosea?” Mungu aliniahidi, huko nyuma, nikiwa mtoto mdogo. Hiyo ndiyo sababu.

³²⁴ Unasema, “Je! hivi huogopi kukosea?” Kamwe siogopi. Mimi hukosea daima. Yeye hakosei.

³²⁵ Sineni maneno yangu. Ninanena Yake. Hiyo ndiyo sababu Yako sahihi kila wakati. Unaona? Hiyo ndiyo sababu ninauuliza ulimwengu, “Nionyeseni wakati mmoja ambapo halikutimia. Nionyeseni wakati mmoja, kwa maelfu ya mambo aliyosema.” Hakuna hata wakati mmoja Yeye alishindwa, wala hatashindwa kamwe, kwa sababu ni Mungu, si mwanadamu.

³²⁶ Kwa hiyo, Mungu yuko hapa sasa. Kristo yuko katikati yetu. Yeye yuko tayari kuwapa Roho Mtakatifu kama mko tayari kumkubali. Si kulipa gharama; gharama imelipwa tayari. Gharama iliombwa hii. . . ililipwa alasiri hii, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, kama uko tayari kulikubali. Kama uko tayari, hebu uachilie moyo wako sasa. Ufungue. Toa woga wote, mashaka yote. Inua mikono yako kwa Mungu, useme, “Bwana Mungu, mimi hapa. Ninasimama hapa. Ninasimama katika Jina la Yesu Kristo.”

Nitawaombea. Nanyi ombeni, pia.

³²⁷ Bwana Yesu, katika njia ya unyenyekevu, katika njia ya kujidhili, ninakukabidhi kusanyiko hili lililosimama kwa miguu yao. Ninawakabidhi Kwako, kwa kuwa wamesimama kwa kuitikia wito. Wanatafuta mambo ya kina. Wanatafuta Uzima zaidi, baada ya kusikia ya kwamba Damu ya Yesu inasafisha kabisa, kwamba hakuna tena cha zaidi; kwamba Neno kamili la Mungu linakaa ndani yao; kwamba amri yenyewe hasa ya sauti yao wenyewe ni nguvu za kuumba, kwa maana ndani yao yuko Roho Mtakatifu. Na Roho Mtakatifu huyu ni Muumba. Yeye hufanya mambo, yatukie, kwa maana Yeye hunena Neno. Nalo Neno, likinenwa, linakuwa Mungu katika kitendo.

³²⁸ Na, Bwana, ninaomba ya kwamba utamtuma Roho Mtakatifu juu ya kila mmoja wao sasa hivi. Na uwape, Bwana, katika nguvu za kufufuka za Kristo, mambo wanayoyatamani moyoni mwao; maisha bora zaidi, ubatizo wa Roho. Bwana, na iwe hivyo, kwamba wasikilizaji hawa wataangaziwa nuru, mioyo ya watu itaona ono na kujazwa na nguvu za Mungu. Ninawakabidhi Kwako, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo.

³²⁹ Sasa endeleeni tu kuinua mikono yenu. Endelea kuinamisha kichwa chako katika maombi. Endelea kuujaza moyo wako, ukisema tu, “Bwana, ninakuamini Wewe.”

Nijaze. Nijaze. Niokoe.

Roho wa Mungu aliye hai, nishukie upya.

³³⁰ Mleteni kiongozi wenu wa nyimbo hapa sasa, aongoze wimbo huu, “Nishukie upya, Roho Mtakatifu.”

³³¹ Endeleeni tu, “Msi—msijali. Nitasimama papa hapa, Bwana. Niko mkononi Mwako, kama yule hakim dhalimu. Mimi niko papa hapa.”

(Ubarikiwea, ndugu. Ulifanya kazi nzuri sana, hivi kwamba nataka utuonyoze hapa.)

³³² Simama tu hapo, “Nitasimama kama sanamu ya kuchonga. Nitasimama kama yule mhubiri alivyosimama hivi majuzi usiku darini. Ninasimama hapa, Bwana. Sijali ni nani anayeniangalia. Sijali kama mchungaji wangu yuko hapa. Sijali ni nani. Niko hapa. Ninatafuta kitu fulani. Ninataka jambo fulani litukie kwangu. Uliliahidi. Niko hapa kumpokea. Na kama litafanya kazi kwa wengine, litafanya kazi kwangu. Niko hapa kumpokea. Sitaketi chini. Nimeamua.”

³³³ [Mtu fulani jukwaani anasema, “Wimbo mmoja, ndugu. Wanaupenda. Yeye anataka uje hapa. Sawa?”—Mh.]

³³⁴ Namna hiyo. Dumu moja kwa moja nalo. Endelea tu kuomba, kama kweli unamaanisha jambo hilo, kama kweli unamaanisha hilo. Amina. Limaanishe kweli, kaa papo hapo. Yeye anasimama kando yako. Shikilia, “Niko hapa, Bwana. Sitaondoka. Nitakuamini Wewe. Uliahidi jambo hilo. Sitachukua wazo fulani. Ninamtaka Roho Mtakatifu halisi awe juu yangu. Ninataka Wewe unijaze sasa hivi. Niko hapa, nikingojea.”

³³⁵ Usiache. Endelea tu kuomba. Usijali muziki. Endelea tu kuomba. Hiyo ndiyo shida yetu, leo: tunasikiliza muziki; tunasikiliza kitu kimoja, kingine. Tunapaswa kuwa tukisikiliza Sauti ya Mungu. Endeleeni kusikiliza. Yeye aliahidi Hilo. Kama aliahidi, atalitimiza. Amina.

³³⁶ Ni mara ngapi nimeona! Macho ya watu ishirini na thelathini elfu yakifunguliwa. Ni mara ngapi nimeona! Huko Durban, Afrika Kusini, niliona miujiza mikuu ishirini na tano elfu, wakati mmoja. Watu wakisimama, papo hapo namna

hiyo, mpaka wakaokota malori saba yaliyojaa mikongojo na viti vya magurudumu kutoka kwa wananchi wenye kuvaa mablanketi ambao hawakujua mkono wa kuume wala wa kushoto. Walisimama papo hapo na kumkubali Kristo, kisha wakaondoka wakaenda zao; viwete, vipofu, viziwi, bubu. Kama Yeye atalifanya kwa Mwafrika mweusi, litawafanyaje ninyi mnaodhaniwa kwamba mnaishi katika wakati, katika kanisa, mahali ambapo Roho Mtakatifu anadhihirishwa? Amina.

Nyenyekea, jinyenyekeze, “Bwana, ninaamini. Ninajua jambo hilo. Mimi. . .” Wewe njoo.

³³⁷ Sasa, kuna kasoro fulani. Na hakuna kosa lolote kwa Mungu. Mungu aliahidi jambo hilo.

³³⁸ Kwa hiyo nisaidie, ningeweza kusimama papa hapa na nishuke niende kwenye marefu ya kanisa moja baada ya mengine, niwaambie, kila mmoja, mahali ulipo na yale uliyofanya. Ninasema hilo katika Jina la Bwana Yesu. Mnajua jambo hilo ni kweli.

³³⁹ Nami ninaona mnaogopa kujiachilia. Mnaogopa jambo fulani. Kuna kasoro fulani. Mungu hafanyi ahadi kisha akaighairi. Ni kweli, papa hapa, kama mnamtaka. Ni juu yenu. Ni kifo chenu; ni mazishi yenu, ni kukubalika kwenu. Hilo hapo Neno.

³⁴⁰ Basi na anisaidie, Roho Mtakatifu yuko hapa. Basi na anisaidie, Yesu Kristo yuko hapa ndani. Je! nimewahi kuwaambia jambo lolote la uongo? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Yeye yuko hapa. Lakini, kuna jambo fulani. Nilikuwa nimesimama pale, nikiangalia Hiyo, kuona Nuru ile ikizunguka kote jengoni hapa, juu yetu, huku na huko tu. Jamani, jamani!

³⁴¹ Haya basi. Ndivyo ilivyo. Ndiyo hivyo. Imemshukia maskini mama fulani hapa. Ndivyo hivyo. Imemshukia mwingine. Haya basi. Hiyo hapo. Sasa, huo hapo wakati wa kumkubali, wakati akiwapo. Unaona? Utukufu! Hakika ingewashukia wengine *pale*. Mungu asifiwe! Naam. Amina. Haya basi. Huyu hapo anaenda, juu ya mtu mwingine hapa sasa, mwingine, mwingine. Mungu asifiwe! Unaona?

³⁴² Yeye ni kweli. Yeye Ndiye Njia, Kweli, Nuru, Uzima. Mkubali wakati anapowashukia wengine. Wakati yuko juu ya wengine, mkubali. Anazunguka, na kuzunguka, na kuzunguka mahali hapa, Roho Mtakatifu anazunguka. Mimi sijasisimkwa. Ninawaambia Ukweli. Utukufu! Hiyo ni kweli.

³⁴³ Dumuni moja kwa moja Naye. Dumuni Naye tu. Dumuni papo hapo. Hamjasimama hapo kwa muda wa dakika tano bado. Bakini papo hapo. “Mungu uliliahidi. Niko hapa kumpokea.” Vema. Huyu hapo. Mpokee, useme, “Ninampokea. Huyu hapa, Bwana. Ninamtaka. Ni—nilisimama hapa juu. Ni nina moyo safi. Ninamaanisha jambo hilo. Wewe uliniahidia Huyu.” Amina. Utukufu! Haleluya!

³⁴⁴ Endeleeeni tu kuamini, endeleeeni kuamini. Mmesema mtaniamini. Roho Mtakatifu, hiyo Nuru, inaendelea kuzunguka hapa na pale jengoni. Ni kitu gani? Anamtafuta mtu ambaye atafungua. Ninawaambia Kweli. Amina.

³⁴⁵ Jaribu kuinua mikono yako, na kumsifu Yeye. Useme, “Bwana, nakushukuru. Ulinipa ahadi. Nitashikilia hiyo ahadi. Nakushukuru, Bwana. Asante.”

Ni—ninaiangalia moja kwa moja. Bwana asifiwe!

³⁴⁶ Mshikilie. Dumu hapo. “Bwana, nitakaa papa hapa. Sijali kama ni asubuhi. Nitakuwa nimesimama papa hapa, nikikusifu. Ninajua utamtuma. Mkutano huu unaisha, usiku wa leo, nami niko hapa bila Roho Mtakatifu. Ninaondoka hapa, nimejazwa na Roho Mtakatifu, kwa hiyo nisaidie. Wewe ulimwahidi Huyo. Nitasimama kama propela-halihewa. Nitafanya lolote unalonitaka nifanye. Ila tu, ninataka Roho Mtakatifu. Nimepania kumpata.”

³⁴⁷ Unapojisalimisha kabisa, Yeye ataingia ndani kikamilifu. Bali mpaka utakapojisalimisha, yeye hawezi kuingia kikamilifu. Jisalimishe. Salimisha mawazo yako. Salimisha fikira zako. Salimisha maisha yako. Salimisha yote. Salimisha hadhi yako. Salimisha kila kitu Kwake sasa. Naye ataingia na kukujaza na Roho Mtakatifu. Yeye yuko hapa kufanya hivyo. Tayari ameshawashukia wawili au watatu hapa jengoni. Kuna zaidi ya hao, wanaomtaka Roho Mtakatifu. Endelea tu kuamini. Utukufu kwa Mungu! Aidha uko sahihi ama umekosea...?... Nyenyekeza mawazo yako mwenyewe. Nyenyekeza njia zako mwenyewe.

³⁴⁸ Kaa tu papo hapo, useme, “Bwana, niko papa hapa sasa. Kama ukimpa mtu mwingine hapa usiku wa leo, utanipa na mimi, pia. Ni—nitakaa papa hapa mpaka Yeye atakapokuja.”

Unapoinua sauti yako, mikono yako, maisha yako, yote uliyo nayo.

Naweza kumsikia Mwokozi wangu akiita,

Inua mikono yako na umwimbie huo.

Ninaweza kusikia...

³⁴⁹ Waliimba wimbo, unajua. “Mwo...” Kama Yeye anakuita uende kwa Roho Mtakatifu, jisalimishe sasa. Salimisha yote uliyo nayo.

Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita,

“Utwa msalaba wako, na ufuate, unifuate Mimi.”

Sasa haya basi.

Aniongozako...

³⁵⁰ “Aniongozako, nita... Uliniongoza umbali huu, Bwana, kwa miguu yangu. Mimi huyu nimesimama.”

...-fuata,
Aniongozako...

[Ndugu Branham anazungumza na ndugu Shakarian—Mh.]

Aniongozako...

³⁵¹ Nimemwonyesha Ndugu Demos sasa hivi. Malaika wa Bwana alipita. Nikasema, “Mwangalie *yule* mwanamke.” Wakati alipopita, aliinua mikono yake namna *hiyo*. Tumeonyesha, Ndugu Demos alimwona, wakati alipokuwa akipita sasa hivi, kwenda kwa mwanamke mmoja papa hapa. Nilisema, “Ndugu Demos, hivi huwezi kumwona? Anazunguka-zunguka tu, kote jengoni.” Nilisema, “Mwangalie wakati alipopita *hapa*.” Maskini bibi huyo alitupa mikono yake juu.

³⁵² Ni maskini yule bibi anayesimama, akiwa amevaa kama kitu chenye vijumbavijumba. Sasa hivi Kitu fulani kimemshukia, dakika chache zilizopita, naye akainua mikono yake. Hiyo ni kweli, mama? Papa hapa tu, akiwa ameinua mikono yake juu, hapa nyuma ya mama huyu aliyevaa gauni la bluu. Yule pale. Unaona? Mbona, hajamaliza... ninamwangalia moja kwa moja. Sasa, kama nimepata kuwaambia jambo lolote ambalo ni makosa, niambieni ni lini. Yuko hapa.

³⁵³ Rafiki zangu, i—inawabidi mtoke kwenye njia hiyo kavu ya Kipentekoste. Inakubidi ufe kweli kweli. Inakupasa kumaanisha jambo hilo kweli kweli. U—una kitu fulani, u—una njaa kwa sehemu, bali si njaa halisi. Huna budi kulifanya halisi. “Petro alipokuwa akisema Maneno haya, Roho Mtakatifu aliwashukia wale waliolisikia.” Jaribu kufunga macho yako na—na kuinamisha kichwa chako. Wazia jambo hilo. Kuna kasoro yoyote? “Bwana, ondoa kutokuamini kwangu.”

³⁵⁴ Sasa hapa, kwa macho ya kibinadamu... Malaika wa Bwana, Ambaye picha yake iko miongoni mwetu, imepigwa na thibitisho la sayansi, Nguzo ile ile ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli. Hiyo ilikuwa ni Yesu, wakati alipokuwa amekufa, akazikwa, akapaa juu kurudi kwa Mungu.

³⁵⁵ Sauli, alipokuwa akienda zake Dameski, alipigwa akaangushwa na Nguzo hiyo hiyo ya Nuru. Akasema, “Bwana, U Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.”

Yesu akasema, “Nimetoka kwa Mungu, na nilienda kwa Mungu.”

³⁵⁶ Ndiye huyu hapa, leo, Yesu yule yule, ameonekana miongoni mwetu kwa macho, akapigwa picha na kamera, akidhihirishwa katika Roho. Loo, ndugu, dada, Mungu anaweza kufanya nini zaidi? Ile saa ya neema!

³⁵⁷ Ninataka kuamini ya kwamba wewe ni mwaminifu. Ninaamini ya kwamba u mwaminifu, bali unajifungia. Wewe si mwaminifu vya kutosha kumpokea. Ni-...

358 Kwa hiyo nisaidie, yuko papa hapa jengoni. Sisemi uongo.

359 Sasa, wakati mnapojituliza kwa muda kidogo. Je! kuna mtu yeyote ndani hapa amejisikia wali—walimpokea Roho Mtakatifu? Pu—punga mkono wako, huku na huko. Nimemwona, kila mahali, juu ya watu. Kubarikiwa. Kubarikiwa. Je! nyote mlibarikiwa? Amina. Wawili, hao ni watatu. Vema. Wanne. Vema. Wako wanne waliompokea Roho Mtakatifu wakati wa bubujiko hilo. Watu wanne walimpokea Roho Mtakatifu wakati huo. Asi-. . . Mungu asifiwe. Unaona?

360 Sasa, muda mfupi tu uliopita, alikuwa akisafiri. Nuru ilikuja ikatokea upande *huu*, ikarudi upande *huu*, ikaenda *hapa*, kisha ikarudi tena. Nikamwambia Ndugu Shakarian, “Njoo hapa. Njoo hapa. Hapa, hapa, hebu iangalie ikija, papa hapa. Ninaitazama inapopita. Kuna maskini bibi fulani pale.” Na mara tu niliposema, “Iko moja kwa moja juu ya maskini bibi yule.” Mnamo wakati huo, akatupa mikono yake juu, akaanza kupiga mayowe. Ilikuwa iko hapo. Unaona? Ikapita tu moja kwa moja, ikaenda moja kwa moja kwenye kona ile, ikarudi moja kwa moja kuzunguka upande *huu*. Siioni sasa. Unaona? Hiyo ni kweli kabisa. Ninawaambia kweli. Unaona? Nayo hii hapa, unaona wanne walipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.

361 Sasa, kama unautaka, ni wako. Ni wako kama uko tayari kujiweka wazi.

362 Sasa ninyi—ninyi mna wa—wa—wazo la yale ambayo mnapaswa kufanya. Kwa namna fulani mna wazo, “Vema, sasa, kama nitasimama hapa juu, *hivi*.” La, la. Hilo, hilo linaninii. . . Unaweza kuketi. Haileti tofauti yoyote uko wapi. Lakini pale utakapojifanya wazi, ndipo Roho Mtakatifu atakapokushukia.

363 Halafu, vema, wakati mwingine Yeye anaanza kukutia mafuta, nawe hutasonga mbele tu pamoja Naye. Unahofu kidogo. Unaogopa. Unaghairi. Jisalimishe tu, jisalimishe kwa Roho Mtakatifu.

364 Usiogope ushupavu wa dini. Kama ni ibilisi anayetenda hivyo, je! hudhani kwamba tutajua jambo hilo? A-ha. Ndio, bwana. Hatukuja hapa. Usihofie jambo hilo. La. Ha—hatawasumbua.

365 Wewe jisalimishe tu kwa Roho Mtakatifu. Unapojisikia umebarikiwa hivyo. . . Kama alivyosema maskini mhudumu huyu kwamba alibarikiwa usiku ule, akiwa amesimama, ambapo kitu fulani chenye joto kilikuja juu yake. Laiti angalijua tu jinsi ya kujisalimisha wakati huo. Hivyo tu. Wewe sema tu “Bwana Yesu, ninakuamini. Ninakukubali.” Ndipo kitu fulani kitaanza kutukia. Unaona? Maanisha jambo hilo kutoka moyoni mwako, ndipo kitatukia. Loo!

366 Je! mnampenda [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mungu awe pamoja nanyi. Mungu awasaidie. Ninataka mninii. . .

367 Ni wangapi wengine zaidi hapa ndani wanaomtaka Roho Mtakatifu? Hebu na tuone mkono wako. Ni wangapi? Moja, mbili, tatu, nne. Loo, jamani, jamani! Hakuna haja ya kwenda bila kumpata Yeye. Kuna wanane ama kumi hapa, kumi na mmoja. Kama kumi na mmoja, kumi na wawili, pengine, hapa ndani, wanaohitaji Roho Mtakatifu, bado. Hebu... Ninajua huenda tunachelewa, labda saa tatu na nusu ama kitu kama hicho. Lakini tuna—tuna wakati mwingi. Tuna wakati mwingi tu. Tunataka wewe uokolewe, rafiki. Tunataka wewe ujazwe. Kumbuka, u—umeokolewa, bila shaka. Unapomkubali Kristo, umeokoka. Bali hujaongoka mpaka umempokea Roho Mtakatifu. Sasa, unajua jambo hilo. Hiyo ni kweli.

368 Yesu alimwambia Petro, ule usiku wa kusalitiwa. Alikuwa ameokoka tayari. Kasema, “Sasa, ukiisha kuongoka, watie nguvu ndugu zako.” Hiyo ni kweli. Loo, hakika. Ulimkubali Kristo kama Mwokozi Wako. Lakini unapoongoka, ndipo unapobadilika kweli. Hiyo ni kweli. Naye hakuwa amebadilika bado. Yeye alilaani mbele za Bwana, na kumkana, na kila kitu. Lakini baada ya kuongoka kwake: “Ukiisha kuongoka, watie nguvu ndugu zako.” Hiyo ni kweli. Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hivyo ndivyo Maandiko yanavyosema, hata hivyo. Hilo linalifanya kuwa kweli. Yesu alimwambia Petro, ambaye alikuwa amemfuata, na kutoa pepo, na kufanya miujiza, na kila kitu, kasema, “Hujaongoka bado. Lakini ukiisha kuongoka, basi watie nguvu ndugu zako.” Vema. Ni kweli. Sasa, kwa nini usinini.

369 Mbona, ungewezaje kukataa mwa—mwa—mwaliko kama huo? Ni kwa ajili yako. Sitaki kukuona ukiondoka hapa bila kumpata Yeye, ndugu. Huenda tusiwe na mkutano mwingine. Hatujui. Hatujui mambo ya mbele. Huenda kamwe tusiwe na mwingine. Kama ukitaka kuketi kitako, na uombe kwa muda kidogo. Ni juu yako. Ni chochote unachotaka kufanya, kama ukitaka kuketi chini, unataka kubaki umesimama. Tutaomba tena. Fanya kila kitu kidogo unachotaka kufanya, bali ninataka umpokee Roho Mtakatifu. Sasa, Yeye ni kwa ajili yako. Kwa nini wanne wampokee papa hapa, na ninyi wengine msimpokee? Unaona? Inakubidi tu kujinyenyekeza, fungua moyo wako na—na uamini kweli kweli jambo hilo.


370 Huenda mimi nisiwe mwalimu mzuri katika jambo hili. Huduma yangu ni ya kuombea wagonjwa.

371 Yuko wapi mhubiri Mpentekoste hapa, mtu fulani, Mhubiri wa Kipentekoste? Inua mkono wako juu. Ni vipi kuhusu jamaa *huyu* hapa, aliyewaombea wagonjwa, huyu aliyeko upande huu hapa? Njoo hapa. Huyu hapa mtu. Ni—nilizaliwa katika majira yasiyo yangu, katika makundi ya Kipentekoste. Lakini, hapa, nataka mtu *huyu* hapa awaombe. Nitasimama kando yake. Mungu akubariki, ndugu.

³⁷² [Ndugu huyo Mpentekoste anakuja mimbarani, na kuwaambia hao wanaosimama, “Kama mtampa nafasi Roho Mtakatifu ashuke juu yenu, inueni mikono yenu.” Ndugu yuyo huyo sasa ananena kwa lugha sentensi sita fupi katika lugha nyingine, kisha anatoka mimbarani na kuendelea kunena katika lugha nyingine, miongoni mwa wanaotaka ubatizo wa Roho Mtakatifu—Mh.]

³⁷³ Iweni na uchaji sasa. Yeye ameshuka kwenda kumwekea mikono mtu fulani. Unaona? Iweni tu na kicho. Msi—msiangalie huku na huko. Endeleeeni kuangalia juu, kuangalia juu, kuangalia juu. Tutaendelea kuomba. Endeleeeni kuomba.

³⁷⁴ [Ndugu Branham anaongea na ndugu mwingine—Mh.] Njoo hapa, ndugu. Wewe chukua mahali pangu, ndugu, hapa. Unaweza kuwaelezea jambo hilo. Unaona? Unajua mengi zaidi juu ya jambo hilo kuliko nijuavyo mimi. Vema. Hebu njoo tu, hebu lieleezee. Wameombea hilo na wanakuja madhabahuni sasa. [Ndugu Branham anaongea na mtu fulani.] Naam.

³⁷⁵ [Ndugu Branham anaongea na ndugu mwingine ambaye amekuja madhabahuni—Mh.] Vema, bwana. Mungu akubariki. Sasa unajua jinsi ya kulifanya hili vema zaidi kuliko mimi. Nitasimama hapa na kuomba. Unaweza kuwapa maelekezo zaidi. Na... 

MUNGU AKIJIFICHA KATIKA URAHISI SWA63-0412E

(God Hiding Himself In Simplicity)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, tarehe 12 Aprili, 1963, kwenye mkutano wa Kimataifa wa Ushirika wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Moteli ya Mbingu za Magharibi huko Albuquerque, New Mexico, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org